**Makonda** azuru kaburi la JPM, atoa machozi



UKURASA 3

**Ushahidi** kesi mauaji dada wa Bilionea Msuya wafungwa rasmi

UKURASA 4



MAKALA MAALUM

**Mjadala** kuhusu ufisadi ni faida ya uwazi wa Rais Samia

UK. 8




UKURASA 11

Nipashe

Jumamosi Novemba 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581491

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

# Muswada mabadiliko NEC watinga bungeni

• **Wajumbe** kufanyiwa usaili, wadau wasema kilio kimesikika... *Uk. 2*



**"Suala la kupita bila kupingwa tumechelewa sana kuachana na hiki kitu. Unaitwa uchaguzi sasa na kama hujachaguliwa unaongozaje?"** – Askofu Dk. Bagonza.



**"Hatua hii inarejesha matumaini ya wananchi... ni mabadiliko yanayofanyika kwa utashi mkubwa na haya tunayoyaona ni kurejesha mifumo ya kidemokrasia nchini."** – Dk. Kitima



**"Tumeambiwa wajumbe watakuwa wanaomba na kufanyiwa usaili Rais atapelekewa majina ya kuteua wajumbe ambao watakuwa makamishna."** – Zitto Kabwe.



**Mapendekezo haya yatachochea ushiriki wa wanawake kwenye nafasi za uongozi kwenye marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa, katiba zao zizingatie jinsia."**- Neema Lugangira.



Rais Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Rais wa Burundi, Évariste Ndayishimiye, pamoja na Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Saudi Arabia na Nchi za Afrika, jijini Riyadh, jana. **Habari uk. 3 PICHA: IKULU**

## Wakuu mashirika umma kupatikana kwa ushindani

UKURASA 3

## Mawakili 10 wajitosa kusuka rufani mama nyama ya swala

UK. 2

**MICHEZO** **YANGA: TUTAIADHIBU ZAIDI SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Baadhi ya viongozi mbalimbali wakiwemo wa dini na kisiasa wakitambulishwa walipofika kwa ajili ya kusikiliza muswada wa marekebisho ya sheria za vyama vya siasa wa mwaka 2023, uliosomwa kwa mara ya kwanza Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Muswada mabadiliko NEC watinga bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewasilisha miswada mitatu bungeni inayopendekeza mabadiliko katika masuala ya kisiasa na uchaguzi ikiwamo muundo mpya wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Muundo mpya wa NEC unapandekezwa kuwa na kamati maalum itakayosaili wajumbe na mkurugenzi wa uchaguzi na siyo kuteuliwa na Rais bila kuomba. Pia inapendekezwa kufutwa kwa utaratibu wa kupita bila kupingwa kwa mgombea na badala yake apigiwe kura ya ndiyo au hapana.

Vilevile, inapendekezwa kila chama cha siasa kuwa na sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalum na maandamano ya vyama vya siasa kufanyika kwa kuzingatia Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi.

Katika miswada hiyo ambayo ilisomwa jana kwa mara ya kwanza, Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023, unapendekeza Kamati ya Usaili kupokea na kufanya uchambuzi wa maombi ya watu wanaoomba kuteuliwa kuwa wajumbe (makamishna) na kupendekeza majina ya wenye sifa kwa Rais kwa ajili ya uteuzi. Mjumbe atakayeteuliwa atatumikia nafasi hiyo kwa miaka mitano.

Inapendekezwa kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kuteuliwa na Rais kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika Ibara ya 74 ya Katiba na watapaswa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu au ya Rufani au wenye sifa ya kuwa mawakili na wawe katika sifa hizo zaidi ya miaka 15.

Sheria inayopendekezwa inaweka utaratibu wa Rais kuunda kamati ya uchunguzi endapo anaona inafaa, ambayo itachunguza na kumshauri ipasavyo kuhusu kuondolewa kwa mjumbe wa tume hiyo.

**CHOMBO HURU**

Inapendekezwa Tume itakuwa na chombo huru na kinachojitegemea na uamuzi wake hautaingiliwa na chombo chochote au kufuata maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya serikali au maoni ya chama cha siasa.

Kama sheria hiyo itapitishwa, Mkurugenzi wa Uchaguzi atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na tume na atakuwa raia wa Tanzania wa kuzaliwa. Sifa nyingine ni kuwa mtumishi wa umma mwandamizi, mwaminifu na mwadilifu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka ya juu katika chama cha siasa.

**GHARAMA ZA UCHAGUZI**

Katika Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi, inapendekeza kuondolewa sharti la vyama vya siasa kuwasilisha stakabadhi halisi za matumizi ya gharama kwa Msajili wa Vyama vya Siasa bali zibaki kwenye vyama kwa ajili ya kuwasilishwa kwa mkaguzi.

Pia imependekezwa kumekwa adhabu dhidi ya chama cha siasa kitakachoruhusu mtu asiye raia wa Tanzania kushiriki katika kufanya uamuzi ndani ya chama husika. Lengo ni kukomesha vitendo vya watu wasio raia kuingilia uamuzi wa vyama vya siasa.

Inapendekezwa pia kuondolewa kwa takwa la wagombea kuwasilisha taarifa kuhusu timu za kampeni kwa wakurugenzi wa halmashauri, makatibu tawala wa wilaya na maofisa watendaji wa kata. Badala yake, imependekezwa ziwasilishwe kwa wasimamizi wa uchaguzi na wasimamizi wasaidizi.

Marekebisho mengine ni kuboreshwa utaratibu wakuchukua na kuwasilisha fomu za tamko la gharama za uchaguzi, zichukuliwe kwa wasimamizi wa uchaguzi wakati mtia nia anachukua fomu za kuomba uteuzi na kuwasilishwa wakati wa kurejeshwa fomu za uteuzi.

Lengo la mapendekezo ya mabadiliko hayo ni kutoa muda wa kutosha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kupitia taarifa zinazowasilishwa na watia nia kuhusu gharama wanazokusudia kutumia kabla hawajaanza kampeni.

**MKUTANO MKUU WA CHAMA**

Katika mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa, inapendekezwa mkutano mkuu wa chama kukasimisha jukumu la kuteua mgombea urais wa Zanzibar. Lengo ni uteuzi wa mgombea huyo kufanywa na halmashauri kuu ya chama.

Kwenye muswada huo, vyama vya siasa vinaruhusiwa kushirikiana hata wakati wa uchaguzi mdogo kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika sheria.

Pia kumeongezwa takwa kwa chama cha siasa kuwasilisha nakala ya kanuni zake wakati wa maombi ya usajili wa muda na kumewekwa kifungu cha kukinyima sifa ya kusajiliwa endapo katiba na kanuni zinaruhusu matumizi ya lugha inayoweza kuhatarisha usalama wa nchi.

**SHERIA MOJA UCHAGUZI**

Inapendekezwa kutungwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2023 ambayo inakusudia kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa.

Hatua hiyo inalenga kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa masharti yote ya sheria hizo ambazo hutekelezwa na mamlaka moja ambayo ni tume.

**KAULI ZA WADAU**

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, alipongeza serikali kwa kutimiza ahadi ya kuleta miswada hiyo bungeni ambayo ilitoa katika Jukwaa la Wadau wa Demokrasia lililofanyika Dar es Salaam.

"Suala la kupita bila kupingwa tumechelewa sana kuachana na hiki kitu. Unaitwa uchaguzi sasa kama hujachaguliwa unaongozaje?" alisema.

Kiongozi wa ACT - Wazalendo, Zitto Kabwe alisema: "Tumeambiwa wajumbe watakuwa wanaomba na kufanyiwa usaili kama Kenya na Afrika Kusini na Rais atapelekewa majina ya kuteua makamishna wa tume."

Zitto alitoa wito kwa wadau wa demokrasia nchini kutumia miezi mitatu iliyopo kushirikiana na Kamati ya Bunge kuboresha miswada hiyo.

Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC), Dh. Charles Kitima, alisema Tanzania kwa mara ya kwanza imeamua tume iundwe kwa kuwa na sheria yake na taasisi za dini zilikuwa zinaona kulikuwa na upungufu mkubwa kutokuwepo sheria hiyo.

"Hatua hii inarejesha matumaini ya wananchi na serikali na pale Rais aliposema 4R ni mabadiliko yanayofanyika kwa utashi mkubwa na haya tunayoyaona ni kurejesha mifumo ya kidemokrasia nchini. Tumuunge mkono Rais," alisema.

**MAONI YA WABUNGE**

Mbunge wa Tandahimba, Katani Katani alisema mabadiliko ya NEC yanalenga kufanya Tume kuwa huru na kwamba malalamiko ya muda mrefu ya Watanzania hususan vyama vya siasa. Mbunge wa Viti maalum, Neema Lugangira alisema mapendekezo hayo yatachochea ushiriki wa wanawake kwenye nafasi za uongozi kwa kuwa kwenye marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa ambapo inataka vyama kwenye katiba zao kuweka kuzingatia jinsia.

# Mawakili 10 wajitosa kusuka rufani mama nyama ya swala

**Na Francis Godwin,** IRINGA

CHAMA cha Mawakili Tanganyika (TLS) Mkoa wa Iringa kimewasilisha Mahakama Kuu Kanda ya Iringa barua ya notisi ya rufani kwa ajili ya mjane Maria Ngoda aliyefungwa jela miaka 22 kwa kosa la kukutwa na vipande 12 vya nyama ya swala kinyume cha sheria.

Katika rufani hiyo, mawakili 10, akiwamo wakili mwanamke Jane Massey ni mmoja wa watakaomtetea ngoda. Pia atakuwamo Wakili Mchungaji Joshua Chusi.

Mwenyekiti wa TLS Mkoa wa Iringa, Wakili Moses Ambindwile, akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, alisema tayari wameshaandika barua ya rufani ambayo imeshafailiwa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Iringa tangu Novemba 8, mwaka huu.

Alisema kinachofuta ni kufaili mahakamani hati ya rufani na kwamba hadi jana usiku, jopo la mawakili 10 kutoka TLS Iringa, walikuwa wamejifungia kuandaa sababu za rufani hiyo. Hati ya rufani itapelekwa mahakamani Jumatatu ijayo.

Kwa mujibu wa Ambindwile, mwitikio wa mawakili wa kujitolea kumsaidia mjane huyo katika rufani yake umekuwa mkubwa kwa kuwa hadi jana mawakili 10 walikuwa wamejitokeza.

"Mawakili watakaohusika katika maandalizi yote ya rufani hadi usikilizaji ni Ambindwile, Dk. Rwezaula Kaijage, Frank Ngafumika, Barnabas Nyalusi, Jane Massey, Samson Rutebuka, Wakili Mchungaji Chusi, Innocent Kibadu, Cosmas Kishamawe na Jali Mongo," alisema.

Ambindwile alisema wanaendelea na jitihada zao kumtetea Maria ikiwamo utafiti kuhusu kesi hiyo na kuandaa sababu za rufani ili hadi kufikia Jumatatu ziwasilishwe mahakamani.

Aliitaka jamii ambayo imeguswa na kesi hiyo kuwa na subira kwa kuwa mchakato wa rufani unaendelea na kusubiri kuona mahakama itaamua nini baada ya rufani hiyo.

Alisema, pamoja na rufani hiyo kitakachoamuliwa na mahakama ndio utakaokuwa uamuzi sahihi kwa kutegemea majadiliano ya pande mbili za mawakili watetezi wa TLS na upande wa mahakama.

## HABARI KITAIFA



Mkazi wa Msigani Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo, akiangalia nyumba iliyoharibiwa na maji jana, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakuu mashirika ya umma kupatikana kwa ushindani

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

SERIKALI imewasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2023 ambao pamoja na mambo mengine umeeleza kutakuwa na utaratibu wa ushindani katika kupata majina ya viongozi watakaoongoza mashirika ya umma ambayo serikali ni mmiliki pekee.

Muswada huo ulisomwa jana kwa mara ya kwanza bungeni na kuwataja baadhi ya viongozi hao ni watendaji wakuu wa mashirika ya umma, wenyeviti au wajumbe wa chombo cha usimamizi.

Pia ulibainisha kuwa mamlaka itajiridhisha kuwa kila mtu aliyependekezwa ana ujuzi unaohitajika katika kusimamia shirika la umma husika, hashiki nafasi ya mwenyekiti katika mashirika zaidi ya mawili au mjumbe katika vyombo vya usimamizi zaidi ya vitatu.

Kwa mujibu wa muswada huo, atakayependekezwa atakuwa na sifa stahiki zilizoainishwa katika sheria husika.

"Bila kujali masharti mengine ya kifungu hiki, endapo nafasi inayokusudiwa kujazwa ni ya mwakilishi wa taasisi au mtu husika, mamlaka itatekeleza wajibu wake chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa kushauriana na taasisi au mtu anayepaswa kuwakilishwa," ilisema sehemu ya muswada huo.

Muswada huo unasema kwa madhumuni ya kuwezesha uteuzi au ujazaji wa nafasi zilizo wazi kwa wakati, mamlaka itahakikisha majina yaliyopatikana ya watu wenye sifa za kuteuliwa, yanawasilishwa kwa mamlaka ya uteuzi ndani ya miezi sita kabla ya kwisha kwa muda wa kuhudumu wa mtu anayeshika nafasi inayokusudiwa kujazwa.

Pia unaeleza kuwa mtu hatakuwa na sifa ya kuteuliwa kama mwenyekiti au mjumbe katika chombo cha usimamizi wa shirika la umma kama ni waziri, katibu mkuu, mbunge, mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya au diwani.

Aidha, muswada unaeleza kuwa mtu yeyote ambaye mara baada ya kuanza kutumika kwa sheria anashika nafasi ya mwenyekiti au mjumbe katika chombo cha usimamizi, atamalizia muhula wake katika nafasi anayoshika, isipokuwa kwamba hatakuwa na sifa za kuteuliwa tena.

"Mamlaka inaweza kumtaka mtendaji mkuu, mwenyekiti au mjumbe wa chombo cha usimamizi au ofisa wa shirika la umma kuwasilisha taarifa yoyote kwa utaratibu na ndani ya muda utakaoainishwa kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka," ulieleza muswada huo.

Pia muswada unaeleza kuwa endapo mtendaji mkuu, mwenyekiti au mjumbe wa chombo cha usimamizi au ofisa wa shirika la umma, bila sababu za msingi atashindwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) ndani ya muda ulioainishwa au atatoa taarifa za uongo au za kupotosha, Mkurugenzi Mtendaji anaweza kupendekeza uamuzi kutolewa.

Uamuzi huo ni kwa mamlaka ya uteuzi kumwondoa madarakani mtendaji mkuu au mwenyekiti au mjumbe wa chombo cha usimamizi. Nyingine ni hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya ofisa wa shirika la umma.

# Makonda azuru kaburi la JPM, atoa machozi

**Na Beatrice Shayo, Chato**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amejikuta anatokwa na machozi alipozuru kaburi la aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, Chato mkoani Geita.

Makonda ambaye wakati wa utawala wa Magufuli alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema hawezi kumkana kiongozi huyo hata akielekezewa bastola. Jana, Makonda alitembelea kaburi hilo na kuongoza sala fupi akiwa anamwombea.

"Magufuli alikuwa mtumishi mwema. Mungu endelea kuitia moyo familia yake kwa kukumbusha katika mema yake aliyoyafanya katika taifa hili, yakawape nguvu na kuwafariji wanapopita usiku na mchana," alisema Makonda

Alisema wananchi wa Chato wasijisikie wanyonge bali wamtazame Mungu kama tumaini lao na nguvu katika maisha. "Ndugu zake na jamaa zake si kwamba walijiandaa bali walijua ya kwamba Mungu yupo basi aendelee kuwalinda. Katika nafasi yangu nitaendelea kumuenzi Dk John Magufuli," alisema huku akitokwa na machozi.

"Kwangu alikuwa mwema, mwalimu mwema, rafiki na baba. Sitamkana kwa gharama yoyote kwa sababu pia Mungu alimpenda. Asante Mungu kwa pendo lako na hakika nitamuenzi katika maisha yangu. Lihimidiwe jina lako mfalme wa mbinguni. Najua hanisikii lakini kwa kuwa wewe unasikia endelea kuwa sehemu ya utumishi wetu.

"Magufuli ninakuahidi kama unaweza kunisikia Rais Samia (Suluhu Hassan) amenipa nafasi nitakuwa msema kweli. Nitakuwa mwaminifu kwa taifa langu na kwa chama changu na huko uliko uendelee kuniombea. Ile kazi uliyotamani ifanyike katika taifa hili chini ya jemedari uliyemwachia nitakuwa sehemu ya kumsaidia, nitamtia moyo. Kupitia hili nina imani taifa litanufaika zaidi," alisema katika maombi yake.

Makonda alisema kwa kuwa Magufuli alilipenda taifa, anamwahidi yeye na kizazi chote kuwa wazalendo na kulilinda na siku wakitawaliwa na wao watahakikisha wanaacha alama.

"Siwezi kumkana Dk. Magufuli hata niwekewe bastola. Wako ambao wanaongea mabaya na kutoa habari za uzushi. Siwezi kumkana, natambua mchango wake na alama aliyoiacha," alisema.

Makonda alisema kumekuwa na kasumba mtu akifa anasemwa vibaya wakati kuna makosa ambayo wanayafanya wenyewe na kumsingizia marehemu na wakati huo huo mazuri yake hawayaelezi.

Makonda alisema anajua mchango wa Dk. Magufuli, uaminifu wake na alama alizoziacha katika taifa na kama kuna mtu anamchonganisha Rais Samia na Dk. Magufuli, aache tabia kwa kuwa wanaheshimiana.

# Samia: Afrika ina kila sababu kuwa kitovu cha chakula

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema Afrika ina kila kinachohitajika kuwa kapu la chakula duniani huku akisisitiza uwekezaji mkubwa na uboreshaji wa sekta ya kilimo.

Aliyasema hayo jana katika mkutano wa Saudi Arabia na Nchi za Afrika uliofanyika Riyadh, Saudi Arabia, ukihusisha wakuu wa nchi kutoka zaidi ya mataifa 50.

Mkutano huo ulijadili kupata majawabu ya namna ya kukuza uhusiano kati ya Saudi Arabia na nchi za Afrika kwenye masuala ya siasa, usalama, uchumi, utafiti, teknolojia na kukuza uwekezaji kwa manufaa ya wananchi.

Katika hotuba yake, Rais Samia alisema Tanzania imeweka ajenda ya kukuza sekta ya kilimo kutoka asilimia tano hadi 10 ifikapo mwaka 2030 pamoja na kuongeza bajeti kutoka dola milioni 88 mwaka 2020 hadi dola milioni 420 mwaka 2023.

"Tunaona Saudi Arabia imeamua kushirikiana na Afrika katika maendeleo ya rasilimali watu. Julai, mwaka huu, Tanzania iliandaa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika wa Rasilimali Watu ambao ulisisitiza umuhimu wa uwekezaji katika rasilimali watu hasa vijana.

"Nia yetu ni kuona ushirikiano huu mpya wa Afrika na Saudia unajengwa juu ya dhamira ya Afrika kwa kuhamasisha rasilimali kuelekea maendeleo ya rasilimali watu," alisema.

Kupitia mkutano huo kulisisitizwa haja ya kuwapo kwa programu za elimu ili kuendesha mageuzi ya kijamii barani Afrika, hivyo kuashiria zaidi kujitolea kwa Saudi Arabia katika kuimarisha uhusiano wake na nchi za Afrika.

Katika hotuba ya ufunguzi, Waziri wa Fedha wa Saudi Arabia, Mohammed Al-Jadaan, alisema Saudi Arabia na Afrika zimekuwa na historia ya pamoja na kuongeza ushirikiano kati ya pande hizo mbili ambao unazidi kukua.

Alisema mkutano huo unalenga kuimarisha zaidi uratibu wa kisiasa, kushughulikia matishio ya usalama wa kikanda na kuimarisha mageuzi ya kiuchumi, hivyo kukuza ushirikiano wa muda mrefu kati ya Saudi Arabia na Afrika.



Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ramadhani Kailima (kushoto) na Mkurugenzi wa Idara ya Uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Mpiga Kura na Tehama, Geofrey Mpangala wakionyesha vifaa mbalimbali vipya (BVR Kits), jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kuchukua na kutunza taarifa za wapiga kura vitakavyotumika kuboresha daftari la mpigakura. Majaribio ya vifaa hivyo yatafanyika kuanzia Novemba 24 hadi 30 mwaka huu kwenye maeneo ya Mkoa wa Mara na Tabora. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ushahidi kesi mauaji dada Bilionea Msuya wafungwa

**Na Grace Gurisha**

KESI ya mauaji ya Aneth Msuya, dada wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya, maarufu kama Bilionea Msuya, imefungwa kusikilizwa baada ya pande zote mbili kufunga ushahidi kwa mashahidi 30 katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Washitakiwa katika kesi hiyo namba 103 ya mwaka 2018 ni mke wa Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wote wakazi wa Arusha.

Katika kesi hiyo, upande wa mashitaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, ulikuwa na mashahidi 25 na utetezi chini ya Wakili Peter Kibatala na Nehemiah Nkoko, ulikuwa na mashahidi watano.

Upande wa utetezi ulifunga ushahidi jana baada ya Muyela kumaliza kuulizwa maswali ya dodoso na jopo la mawakili wa serikali na pia kujibu maswali ya nyongeza kutoka kwa Wakili Nkoko.

Baada ya shahidi huyo kuhitimisha ushahidi wake, Wakili Kimweri aliieleza mahakama mbele ya Jaji Edwin Kakolaki kuwa baada ya wenzao kufunga ushahidi, wanaomba muda wa kufanya majumuisho ya mwisho kwa njia ya maandishi.

Jaji Kakolaki alimuuliza Wakili Kimweri kwamba wapewe muda gani kufanya kazi hiyo na kudai usiopungua wiki mbili.

Baada ya majibu hayo, Jaji Kakolaki aliwauliza Kibatala na Nkoko wanasemaje kuhusu hilo na kujibu kuwa wanaunga mkono hoja zote mbili ndani ya wiki mbili watafaili kwa pamoja majumuisho hayo.

"Kutokana na kukamilika kwa ushahidi wa pande zote mbili kwa kuzingatia hoja zote, majumuisho ndani ya wiki mbili yawe yamewasilishwa mahakamani hapa kabla ya Desemba 2, 2023," alisema Jaji Kakolaki.

Pia Jaji Kakolaki alisema kesi itatajwa Desemba 4,2023 ili kuangalia utaratibu mwingine baada ya hapo.

Baada ya Jaji kutoka mahakamani, mawakili wa Serikali,utetezi na ndugu jamaa na marafiki katika kesi hiyo walikuwa wakipongezana kwa kukumbatiana kwa hatua ambayo wameivuka.

Mchakato wa usikilizwaji wa kesi hiyo, ulianza Novemba, 2021 kutokana na ratiba ya vikao vya mahakama iliyopangwa. Shahidi wa kwanza wa upande wa mashitaka alikuwa Sajenti Mwajuma (42) ambaye ndiye aliyetoa maelezo ya onyo ya Mrita.

Katika maelezo hayo, Mrita anatuhumiwa kudai kuwa aliamua kumuua wifi yake kwa sababu alikuwa anamfuatafuata katika suala la usimamizi wa mirathi ya mumewe na kwamba katika kutekeleza mauaji hayo, alimkodi mtu ambaye alimlipa Sh. milioni 20.

Maelezo hayo ya Miriam yalisomwa mahakamani na shahidi huyo aliyemhoji mshtakiwa na kuandika maelezo yake alipotiwa mbaroni, baada ya kupokelewa mahakamani kuwa kielelezo cha ushahidi wa upande wa mashtaka.

Hata hivyo, Mrita katika utetezi wake alikana maelezo hayo na kudai kuwa kwanza hawezi kumuua wifi yake Aneth kwa sababu alikuwa ni mtoto wake wa kumlea tangu yupo shule ya msingi hadi anaolewa na pia hakuwahi kuwa na ugomvi wa mali au mirathi na wifi yake huyo.

Shahidi wa 25 wa upande wa mashitaka, Getruda Mfuru ambae alikuwa dada wa kazi wa Aneth, alidai kuwa Mrita alimwahidi kumpa Sh bilioni 50 kama akikamilisha kazi ambayo anaitaka kuifanya na dada yake.

Pia alidai kuwa Mrita akiwa na mshitakiwa wa pili, walimfuata mara tatu na kumueleza kwamba kabla ya Mei 25,2016 anatakiwa awe ameshaondoka kwa dada yake ili kukamilisha kazi yao, siku ya kwanza hawakumtishia, lakini siku ya pili na ya tatu walimtishia kwa bastola.

Mfuru akiwa katika kizimba aliweza kuwatambua washitakiwa wote wawili huku akidai kuwa ndiyo hao hao aliowatambua katika gwaride la utambuzi lililofanywa na Jeshi la Polisi na ndiyo aliokuwa akikutana nao nje ya nyumba ya Aneth.

Katika utetezi wa Muyela, kwanza aliyakataa majina ambayo yalikuwa kwenye hati ya mashitaka na kudai kuwa siyo yake na kuhusiana na mauji ya Aneth yeye hakushirikiana na Mrita kumuua licha ya kwamba wanafahamiana.

Hata hivyo, Wakili Kimweri alimtaka mshtakiwa huyo akubalianae nae kwamba aliyekamatwa kwenye kesi hiyo ni yeye na sio mtu mwingine, ambapo Muyela alikubaliana nae kuwa ni yeye.

Kuhusiana na ushahidi wa sahihi yake, Kimweri alitaka kujua kama mshitakiwa ni mtaalamu wa maandishi hadi kufikia hatua ya kukataa sahihi zake, alidai kuwa yeye siyo mtaalamu.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni , Dar es Salaam, alikiri kuhusika na mauaji hayo, katika maelezo yake ya onyo.

# NEC sasa kuanza uboreshaji daftari la wapigakura

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inatarajia kufanya uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapigakura katika Kata ya Ng'ambo, Manispaa ya Tabora na Kata ya Ikoma, Rorya mkoani Mara.

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Ramadhan Kailima, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akitoa taarifa kuhusu uboreshaji wa majaribio wa daftari la kudumu la wapigakura.

Kailima alisema uboreshaji huo unatarajiwa kuanza Novemba 24 hadi 30, mwaka huu, katika vituo 16 vya kuandikisha wapigakura.

"Uboreshaji wa majaribio utafanyika katika vituo 16 vya kuandikisha wapigakura kati ya hivyo, 10 ni vya Kata ya Ng'ambo na sita vipo Kata ya Ikoma. Vituo vya uandikishaji vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni,"alisema.

Mkuregenzi huyo alisema uboreshaji huo wa majaribio unafanyika kwa lengo la kupima uwezo wa vifaa na mifumo ya uandikishaji itakayotumika.

Alisema mifumo hiyo ni ile itakayotumika wakati wa uboreshjai wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unaotarajiwa kufanyika nchi nzima kwa tarehe na ratiba itakayopangwa na tume.

"Uboreshaji wa majaribio utahusisha kuandikisha raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 au zaidi na atakayetimiza umri wa miaka 18 kabla au ifikapo tarehe ya uchaguzi mkuu mwaka 2025.

"Wapigakura wanaoboresha taarifa zao ni wale ambao wamehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda lingine, waliopoteza au kadi zilizoharibika, wanaorekebisha taarifa na kuondoa wapigakura waliopoteza sifa za kuwamo katika daftari," alisema Kailima.

Alisema tume itatumia 'BVR Kits' zenye vifaa mbalimbali vinavyowasiliana ili kuchukua na kutunza taarifa za wapiga kura.

"BVR Kits hizo zimeboreshwa na ni tofauti na zile zilizotumika katika zoezi la uboresaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka 2015 na 2019," alisisitiza Kailima.

Pia alisema tume imesanifu na kuboresha mfumo wa uandikishaji wapiga kura ili kukidhi muundo na 'BVR Kits' za sasa ambazo zinatumia progarmu ya android ambapo BVR za awali zilikuwa zinatumia progaramu ya 'Microsoft Windows'.

Pia alisema mfumo wa uandikishaji ulioboreshwa utawawezesha wapiga kura ambao wameshaandikishwa na wapo kwenye daftari la wapiga kura kuanzisha mchakato wa kuboreha taarifa zao.

Alisema katika uboreshaji huo wa daftari wa majaribio, vyama vya siasa vitashiriki kwa kuweka wakala mmoja mmoja katika kila kituo cha kuandikisha, lengo ni kushuhudia na kujiridhisha kuhusu taratibu zitakazo tumika.

Hata hivyo, alisema utaratibu ulioainishwa wa kuboresha taarifa kwa njia mtandao hautawahusu wapiga kura wanaotaka kuandikishwa kwa mara ya kwanza na wapiga kura ambao kadi zao zimeharibika au kupotea.

"Hawa wanashauriwa wafike kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura na kufuata taratibu watakazoelekezwa na maofisa wa tume watakaokuwapo kwenye kituo. Nitoe wito kwa wakazi wa maeneo haya ambayo zoezi hili litanyika kujitokeza kwa wingi kuitumia fursa hii," alisema.

## Watanzania 50,000 kunufaika viwanda 100

Na Mary Geofrey

WAWEKEZAJI kutoka Misri wamezindua rasmi uwekezaji wenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 400 katika kongani ya viwanda 100 vitakavyojengwa eneo la Mlandizi mkoani Pwani.

Uwekezaji wa kongani ya viwanda 100 wa kampuni Elsewedy Electric, unatarajia kuzalisha zaidi ya ajira 50,000 za mkataba na za moja kwa moja.

Uwekezaji huo ni moja ya matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya Misri mwaka 2021 ambapo aliwahamasisha wawekezaji kuja kuwekeza nchini.

Katika uzinduzi huo ulifanyika hivi karibuni, mjini Cairo na uliokutanisha wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nchini humo na watendaji kutoka Tanzania, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Viwanda wa kampuni hiyo, Eslewedy Mohamed Alkammah, alisema wameendelea kuwekeza nchini Tanzania.

Alisema uwekezaji huo unatokana na Tanzania kuwa na sera nzuri ya uwekezaji pamoja na ushirikiano mkubwa unaotolewa na serikali.

"Tanzania imefungua sera na milango yako ya uwekezaji ndio sababu leo hii tumechagua kuwekeza hapa. Mbali na viwanda hivi tunavyoanzisha mamilioni ya Watanzania watapata ajira kupitia uwekezaji huu," alisema.

Mkurugenzi wa Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gilead Teri, alisema Tanzania imedhamiria kuendelea kushirikiana na wawekezaji kutoka nchini Misri katika kuwekeza kwenye sekta mbalimbali.

Rais wa Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Huru (GAFI) wa Misri, Hossam Heiba, alibainisha kuwa uhusiano wa kiuwekezaji baina ya Misri na Tanzania umekuwa mfano wa kuigwa wa ushirikano wa nchi za Afrika kwenye uwekezaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Elsewedy Electric Afrika Mashariki, Ibrahim Qamar, alisema katika uwekezaji ambao tayari wameshafanya nchini Tanzania ukiwamo wa uzalishaji wa vifaa vya umeme kumekuwa na mafanikio makubwa hasa kwa kupata soko katika nchi za Afrika Mashariki na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Kongani ya viwanda 100 ya Elsewedy ni miongoni mwa uwekezaji wa kimkakati ambao pia, utatumia bandari kavu ya Kwala Pamoja na Reli ya Kisasa ya SGR kwa ajili ya kubebea mizigo.




Mwenyekiti wa Bodi ya Tanga Cement Plc, Patrick Rutabanzibwa (wa pili kulia), akizungumza wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa wanahisa wa kampuni hiyo, jijini Dar es salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanga Cement PLC, Reinhardt Swart (wa pili kushoto), Mkuu wa Divisheni ya Fedha wa kampuni hiyo, Pieter De Jager (kushoto) na Mkurugenzi wa Bodi, Raymond Mbilinyi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EWURA yatoa mbinu kupunguza bei mafuta

Na Joseph Mwendapole

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), imeiagiza Wakala wa Uagizaji Mafuta Pamoja (PBPA), kuhamasisha kampuni nyingi kushiriki zabuni ya uagizaji wa mafuta kwa pamoja ili kuongeza ushindani ambao utasaidia kushusha bei ya mafuta.

EWURA imesema kwa sasa ni kampuni tano tu zinazoshiriki zabuni ya kuagiza mafuta kwa pamoja kati ya kampuni 18 zilizoidhinishwa na mamlaka hiyo hali inayosababisha ushindani kuwa mdogo na kusababisha bei kuendelea kupaa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, James Andilile, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu maendeleo ya masuala ya mafuta, maji na gesi asilia.

Dk. Andilile alisema ushiriki wa kampuni kwenye zabuni ukiwa mdogo ushindani pia unakuwa mdogo hali inayosababisha bei ya mafuta kuendelea kuwa juu.

"Tumemwelekeza PBPA awahamasishe wamiliki wa kampuni zote 18 ziwe zinashiriki mchakato wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja kwasababu tumeona kwa sasa zinazoshiriki ni kati ya tano na nane tu. Kwa hiyo kama ziko 'serious' (makini) kweli lazima tuzione kwenye mchakato wa zabuni ili kuongeza ushindani kwasababu zikishiriki nyingi ndipo mafuta yanashuka bei," alisema

Alisema Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) nalo limeanza kushiriki kikamilifu kwenye mchakato wa kuagiza mafuta kwa pamoja na kwamba mafuta yatakayoletwa mwezi Desemba shirika hilo limeshinda baadhi ya zabuni.

"Baada ya TPDC kuanza kushiriki kwenye mchakato huu, tumeanza kuona mwelekeo mzuri wa bei ya mafuta kuanza kushuka kwa hiyo tutaendelea kuhamasisha kampuni nyingi zaidi zishiriki kwenye zabuni hizi kila mara," alisema Dk. Andilile.

Alisema zamani leseni za kampuni ziliendelea kuwa hai kwa zinapoagiza mafuta hata mara moja ndani ya miezi sita lakini EWURA imeboresha mifumo ya leseni na sasa kampuni ambayo haitaagiza mafuta ndani ya miezi mitatu itapokonywa leseni.

"Utaratibu wa miezi sita ulisababisha kuwa na kampuni nyingi lakini ambazo hazifanyi kazi kwasababu kampuni ikiagiza mafuta hata mara moja tu ndani ya miezi sita leseni yake inabaki kuwa hai sasa tumebadilisha kanuni kwa sasa kampuni ambayo haitagiza mafutaa ndani ya miezi mitatu tu leseni yake itakufa,.

"Pia tumeboresha kanuni kwamba kampuni ya kuagiza mafuta itatakiwa kuagiza mafuta kwa uwiano wa soko lake market share, kama imetengewa asilimia 15 market share basi tukifanya tathimini ya kiasi ulichoagiza basi kiwe hiyo asilimia 15 ambayo ulitakiwa kuagiza 'market share' yako," alisema.

Alisema EWURA inafanyia kazi ushauri wa wananchi na viongozi mbalimbali wanaotaka bei ya mafuta kwenye mikoa yote ilingane na ifanane na mikoa ya jirani na Dar es Salaam.

"Kwenye hili tumeangalia wenzetu Zambia, Ghana, Ethipia na Misri wanafanyaje, lakini hiki siyo kitu kipya wale wa zamani kama mimi mtambuka hiki kitu kiliwahi kufanyika kufanya bei za mikoa yote kulingana na nakumbuka kuanzia mwaka 1985 mpaka 2008 huo utaratibu ulikuwepo ambapo bei za mafuta zilikuwa sawa nchi nzima," alisema.

# Wadau wapendekeza nafasi za uteuzi zishindanishwe

Na Romana Mallya

WADAU wameshauri nafasi za wenyeviti wa bodi na wajumbe wa mashirika na taasisi zilizo chini ya serikali zitolewe kwa utaratibu wa kuomba na watu washindanishwe ili kupata wenye ujuzi, maarifa, utashi wa kufanya kazi wanayoijua.

Katika mahojiano maalum na mwandishi wa habari hizi jana kuhusu nafasi hizo baada ya uteuzi na utenguzi wa mara kwa mara, wadau hao walishauri ili kuwapata watu ambao watakaa muda mrefu katika nafasi hizo ni vyema mfumo wa kuwapata ubadilike.

Wakati ushauri huo ukitolewa, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, Rais Samia Suluhu Hassan, amevunja Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Mchambuzi wa masuala ya kiuchumi, Prof. Haji Semboja, alisema ni lazima kubadilishwe utaratibu wa kupata watu wanaoongoza bodi hizo.

Alisema lengo ni kumpata mtu mwenye ujuzi, maarifa, utashi wa kufanya kazi anayoijua, mchakato wa kumtafuta uwe wazi.

"Mtu atume wasifu wake (CV) nazo ziwe wazi, nafasi zitangazwe wazi na watu waombe, wachujwe katika ngazi mbalimbali za mahojiano, washindanishwe na katika kupewa hiyo kazi mtu aelewe ameomba mwenyewe hivyo anatumikia taifa," alisema.

Alisema ni vyema nafasi hizo zitangazwe ili kuwe na fursa ya watu kuziomba na ziwapo kampuni zinazohusika na masuala hayo.

Pia, alishauri taratibu za kisheria zilizowekwa kutekeleza mashirika hayo, zifuate mfumo wa kimataifa wa mtu katika nafasi awe na elimu, mafunzo, maarifa, ujuzi, uelewa na utashi wa kuifanya kazi hiyo na awe anaielewa. Mtaalam wa uchumi, Dk. Donath Olomi, alisema anaafiki utaratibu uliopo, watu kuomba ingawa haufuatwi kila wakati.

"Taasisi kama hizi TCRA zinahitaji watu ambao ni wenye taaluma, haitakiwi mtu awekwe halafu usikie ametolewa kapelekwa kule. Kunatakiwa kuwe na utaratibu unaoeleweka wa kuteua watu na mtu kama amekosea kuna utaratibu wa kumwajibisha.

"Kukiwa na utaratibu wa mtu kuomba kutasaidia. Pia bodi iwe na mamlaka ya uteuzi na utenguzi yaani hata kama Rais anateua iwe imependekezwa na bodi.

"Lakini mabadiliko yanapotokea kwa namna hiyo inatia mashaka usimamizi wa taasisi itakuaje? Kadri mtu anavyokaa ndipo anaelewa taasisi fulani na kutengeneza maono," alisema.

Taarifa iliyotolewa na Ikulu, ilisema Rais Samia pia amemteua Balozi James Bwana kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Afrika Kusini, akichukua nafasi ya Balozi Meja Jenerali Gaudence Salim Milanzi ambaye amestaafu.

Wengine aliowateua ni Balozi Said Hussein Massoro kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Kuwait, akichukua nafasi ya Balozi Said Shaib Mussa ambaye aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri Tanzanite, JKT Queens michuano Afrika

**WAKATI** Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), imefuzu kucheza fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2024), Simba na Yanga zimetinga hatua ya makundi katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, timu za wanawake pia zimeendelea kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Hii ni mara ya kwanza kwa vigogo hao wa soka nchini, Simba na Yanga zote kutoka jijini, Dar es Salaam kwa pamoja kufuzu hatua ya makundi katika michuano hiyo ya kimataifa inayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mafanikio hayo yanatokana na maandalizi, misingi na mazingira bora yaliyopo na yanayochagizwa na hamasa kutoka kwa shabiki namba moja na kiongozi wa nchi Rais, Samia Suluhu Hassan.

Katika kuendelea kupeperusha bendera ya Tanzania, mabingwa wa soka nchini, JKT Queens inashuka dimbani kukutana na Sporting Casablanca ya Morocco katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa wa Afrika kwa Wanawake utakaochezwa leo nchini, Ivory Coast.

JKT Queens inashiriki mashindano hayo baada ya kutwaa ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), ikiwavua ubingwa ndugu zao, Simba Queens, na ili Maafande hao wasonge mbele katika michuano hiyo wanatakiwa kupata ushindi wa aina yoyote.

Ushindi ndio matokeo pekee ambayo JKT Queens inahitaji ili kutinga hatua ya nusu fainali bila kujali matokeo ya mechi nyingine katika kundi hilo, ambayo itakuwa ya kumalizi hatua hiyo ya awali.

Watanzania wanataka kuona wawakilishi wao wanasonga mbele na kufanya vizuri zaidi katika michuano hiyo ambayo msimu uliopita, Simba Queens ilimaliza katika nafasi ya nne na wenyeji ASFAR ya Morocco ikibeba taji lililokuwa linashikiliwa na Mamelodi Sundwons Ladies ya Afrika Kusini.

Wachezaji na benchi la ufundi la JKT Queens huu ni wakati wa kuonyesha safari yenu ya kufika kwenye michuano hiyo haikuwa ya kubahatisha, hivyo mnatakiwa kucheza katika kiwango cha juu, utulivu na umakini ili kufikia malengo.

Kufanya vyema katika mechi ya leo, sio tu kutaifanya timu yenu isonge mbele, lakini kutawahakikishia kupata kitita zaidi kinachotolewa na CAF kutokana na hatua ambayo mmefika katika mashindano hayo yatakayomalizika ifikapo Novemba 19, mwaka huu.

Tunapenda kuwakumbusha wachezaji kucheza kwa nidhamu ili kutoigharimu timu kuelekea michezo inayofuata endapo mtasonga mbele, lakini kufahamu mashindano hayo ni daraja kwao kwa kuangaliwa na mawakala na makocha kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Hapa nyumbani, kesho Tanzanite itawakaribisha wenzao kutoka Nigeria na ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele, tunawaombea wapate ushindi mnono.

Matokeo chanya ndio yatarahisisha kazi kuelekea mchezo wa marudiano ambao utachezwa wiki ijayo huko ugenini, na kama inavyofahamika 'fitina' za ndani na nje ya uwanja kwa nchi za Magharibi ni jambo la kawaida.

Kila mchezaji ambaye atapa nafasi katika mechi ya leo (JKT Queens) na kesho (Tanzanite), anatakiwa afahamu kufanya kwake vizuri kutasaidia timu kupata matokeo chanya na kutimiza malengo ya nchi ya kubeba mataji mbalimbali msimu huu.

Lakini pia kufanya vyema kwa kila mchezaji katika mechi hizi mbili za kimataifa kutapandisha thamani yake na kujihakikishia namba ya kudumu katika kikosi hicho cha Maafande wa JKT au kwenye timu za taifa (Tanzanite au Twiga Stars).

Mashabiki wa soka na wadau wa michezo nchini wanaitwa kujitokeza kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ili kuishangilia Tanzanite, mchezo huo ukiwa ni bure kwa kila atakayefika uwanjani hapo.

**Kila la heri JKT Queens, kila la heri Tanzanite.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Simba hakuna anayepaswa kulaumiwa, songeni mbele

**KUNA** mparaganyiko unaoitafuna Klabu ya Simba baada ya kukutana na kichapo cha mabao 5-1 kutoka kwa watani zao wa jadi Yanga, walichokipata kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili iliyopita.

Viongozi, wanachama, mashabiki, na hata wachezaji hawazungumzi tena lugha moja kutokana na kichapo hicho cha aibu. Kila mmoja anaongea la kwake.

Namungo FC nao wakaukoleza moto kwa kuilazimisha kutoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, mechi iliyochezwa juzi.

Ukizisikiliza pande zote, kwa vitendo na maneno yao, utagundua mpaka sasa Simba haijui tatizo la kufanya vibaya katika mechi hizo mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ni sawa na binadamu ambaye anaumwa lakini haujui ugonjwa wake. Anachofanya anabahatisha tu, viongozi wakaanza na kumtimua Kocha Mkuu, Roberto Oliveira mara baada ya kipigo hicho cha fedheha.

Ina maana viongozi wao wakaona kocha ndiyo tatizo na akiondoka basi mambo yatakuwa vizuri.

Hapo hapo kuna baadhi ya viongozi ingawa hawajatoka hadharani kusema, lakini wanaamini kuna baadhi ya wachezaji wamehujumu timu yao.

Ndiyo maana suala likafika mpaka bungeni, lakini wakashauriwa kwenda kutoa taarifa rasmi katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kama wana ushahidi wa kutosha.

Baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba wao nao hawaamini kama kocha ndiyo tatizo, bali viongozi ndio tatizo, hasa wale viongozi wakuu kutoka pande mbili za Mwekezaji na Wanachama.

Salim Abdallah 'Try Again', ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi analaumiwa na kutakiwa ajiuzulu, pamoja na Murtaza Mangungu ambaye ni Mwenyekiti wa upande wa wanachama.

Sasa kuna baadhi yao wao wanaamini tatizo ni wachezaji, na si viongozi, hivyo kuwanyooshea video vya shahada wakisema hawajitumi, hawajitoi kuipambania klabu.

Inawezekana kila upande ukawa sahihi kwa wanavyoona, lakini sidhani kama kati ya pande zote kuna yoyote kumnyooshea mwenzake kidole kama ndiyo tatizo.

Binafsi ninavyoona Simba ina tatizo mtambuka, yaani linatoka huku na kuangukia kule, hivyo kila mmoja ana ni sehemu ya matatizo.

Nikianza kuyaainisha, wanachama na klabu hiyo ndiyo waliomweka madarakani Mangungu katika uchaguzi uliofanyika Januari mwishoni, mwaka huu.

Nadhani hapa wanachama wanaanza kuwa tatizo kwa sababu kama waliona hafai wasingemchagua kwa wingi kwa kigezo hatakuwa na jipya, alishaongoza kwa kipindi kadhaa.

Naweza nikawaelewa mashabiki, lakini si wanachama ambao hao hao, ndiyo leo wanasema Mangungu hafai.

Viongozi nao pia wana matatizo. Kikosi tunachokiona cha Simba kina wachezaji tangu wa mwaka 2013 na 2014, lakini bado hadi leo eti ndiyo tegemeo kwenye timu.

Badala yake wanasajiliwa wachezaji wengi wa kukaa benchi, lakini tegemeo la timu ni wale wale miaka nenda rudi.

Inawezekana Djuma Shaaban angekuwa Simba mpaka leo angekuwa anacheza. Hili ndilo kosa au tatizo la viongozi wa Simba hadi kunyooshewa vidole, ni wagumu kufanya mabadiliko. Hii Simba inayoonekana sasa imeshachoka, inahitaji usajili mkubwa wa maana na kubakisha wachezaji wachache vijana na wenye uwezo.

Wachezaji nao sidhani kama wanaweza kukaa kuwanyooshea vidole viongozi kwa sababu wanavyocheza tu wanaonekana baadhi wamezeeka, wapo viwango vyao vimeshuka, wanacheza kama wako katika bonanza, hawakimbii, hawapambani, nao pia ni sehemu ya tatizo.

Ndiyo maana narudia kusema tena kwa upande Simba una matatizo, ukiondoa mashabiki tu ambao hawana sauti au mamlaka ya kufanya lolote, lakini hakuna upande wowote ambao unaweza kujiona wenyewe hauna makosa na kunyoosha kidole upande mwingine.

# Watanzania wengi wanajenga nyumba miaka 18

**Na Romana Mallya**

RIPOTI ya utafiti kuhusu mahitaji ya soko la nyumba za kima cha chini Tanzania imeonyesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanajenga makazi ya muda na wengine huchukua mpaka miaka 18 hadi kumaliza.

Utafiti huo umefanywa na kampuni ya Tanzania Mortgage Refinance Company (TMRC) kwa kushirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali ya kimataifa ya Habitat for Humanity International (HFHI).

Mkurugenzi wa Huduma za Kifedha za Makazi AHFHI Afrika, Daniel Mhina, akizungumza juzi jijini Dar es Salaam wakati wa utoaji wa utafiti huo, alisema ripoti imeonyesha Watanzania wengi wa kipato cha chini na cha kati bado hawana uwezo wa kupata huduma za kifedha kutatua matatizo ya nyumba.

"Zaidi ya asilimia 70 Watanzania wanajenga makazi yao kwa muda na wengine wanachukua mpaka miaka 18 kujenga makazi yao. Sasa miaka 18 na gharama zinavyoongezeka unakuta baada ya miaka 18 nyumba zinakuwa kubwa sana," alisema.

Pia alisema wamegundua kuna matatizo madogo madogo ya nyumba ambayo Watanzania wanahitaji huku akitolea mfano wa marekebisho ya mabati au madirisha na kupaka rangi ambapo mtu anapaswa kupata huduma hizo katika taasisi za kifedha.

Mhina alisema changamoto waliyoiona kupitia utafiti huo, watoa huduma za kifedha hawana mikopo inayoendana na matakwa ya Watanzania.

Alisema katika uzinduzi huo wameziita benki na taasisi zinazotoa mikopo ili kuona changamoto ni zipi na kuangalia maeneo ambayo wanaweza kuyatumia kama fursa ili waje na huduma zinazoendana na hali ya Mtanzania. "Sisi kwa kushirikiana na TMRC tutatafuta wadau wawili au watatu ili kufanya nao kazi ili kutengeneza mikopo kwa ajili ya watu wa hali ya chini na kati ili kuonyesha soko kuwa inawezekana," alisema.

Alitolea mfano nchi ya Kenya imeweza kusaidia watu makazi bora na Tanzania wananchi 400 wamesaidiwa kuwa na mkazi bora kupitia mkopo wa Sh. milioni 190.

Alisema mikopo ambayo wanaongelea ni ya kima cha chini kuanzia Sh. 100,000 hadi Sh. milioni mbili ambapo mtu anapopata dharura hawezi kwenda benki na kuuchukua kwa haraka.

"Kwa sasa ukiangalia watoa huduma wanahitaji vigezo ambavyo ni vigumu ili mtu apate mikopo na hii ni kwa sababu mikopo yao ni ya gharama kubwa. Tunataka tuondoe hizi changamoto za mtu kutakiwa kupeleka vitu vingi sana ili apate mkopo. "Watanzania wengi wameonesha wanataka mikopo ya kujenga nyumba zao mikopo midogo midogo ili kusaidia vitu vidogo vidogo kama marekebisho ya nyumba. Pia ripoti imeonesha Watanzania wanataka riba kiwango gani? Na kulipa kwa kipindi gani? "alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TMRC, Oscar Mgaya, alisema wao katika kutekeleza malengo yao, waliona kuna pengo kubwa kwa watu wa kipato cha kati na cha chini ambao ndio sehemu kubwa ya Watanzania.

Alisema kwa kushirikiana na Habitat ambao wamebobea kwenye utoaji wa fedha kwa watu wa kipato cha kati na cha chini, wakaona wafanye utafiti huo ili kuona mahitaji ndani ya soko.

# Makonda anusa harufu ya rushwa Muleba

**Na Beatrice Shayo,**
MULEBA

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi na Uenezi, Paul Makonda, amesema wilaya ya Muleba mkoani Kagera ina harufu ya rushwa vikiwamo vituo vya polisi, vitalu na ofisi za watumishi wa umma.

Kutokana na kuwapo hali hiyo, amesema atamwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Salum Hamduni, kupeleka timu maalum ya kumaliza tatizo hilo.

Vilevile, ameitaka TAKUKURU kumchunguza aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Mipango Miji wa manispaa ya Bukoba, Catres Rwegasila, ambaye jina lake limetajwa kuhusika katika migogoro ya ardhi.

Akiwa ziarani Muleba jana, Makonda akizungumza na wananchi, alisema kuna mambo matatu likiwamo la kutokomeza vitendo vya rushwa humo.

"Muleba kuna harufu ya rushwa, kuna rushwa kwenye vitalu, kuna rushwa kwenye ofisi za watumishi wa umma na vituo vya polisi. Kuna rushwa katika maeneo mengi nitaongea na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, tulete timu maalum kuhakikisha rushwa sio sehemu ya wilaya ya Muleba," aliahidi.

Kuhusu matatizo ya maji, alisema atazungumza na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ili amweleze mpango uliopo wa kutatua kero hiyo wilayani humo. "Ukiona kuna mahali hapajakwenda sawa ni sisi wasaidizi wake tumeshindwa kutekeleza ndoto yake," alibainisha.

Alisema mambo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan amefanya na fedha alizozipeleka wilayani Muleba zinapaswa zisimamiwe vizuri ili kukamilisha utekelezaji wa ilani ya CCM. "Ndugu zangu wa TARURA (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) mna bahati mvua inanyesha, isingekuwa mvua leo nilikuwa ninakula sahani moja na TARURA. Tunataka barabara zenye ubora.

"Ndugu zangu mnaogawa vitalu mnaohusika na upande wa maeneo ya ufugaji, kuna maeneo tunatakiwa kuyafanyia kazi ya migogoro," alisema Makonda.

Alisema Rais Samia alishatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko, kuboresha afya, kuimarisha elimu na yeye kama msemaji wa chama atahakikisha wanafuatilia fedha hizo ili maendeleo ya wana Muleba yapatikane kwa wakati uliokusudiwa.

Kuhusu Rwegasila aliagiza TAKUKURU kumchunguza mara baada ya kupokea malalamiko ya migogoro ya ardhi ikihusisha ofisi hiyo.

Katika mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye uwanja wa Mayunga ulioko Manispaa ya Bukoba, mkazi wa Kagondo, Florida Christian, alidai tangu mwaka 2005 amekuwa akilalamika kuchukuliwa ardhi yake na ofisa huyo wa ardhi lakini hakutaka kumsaidia.

"Manispaa inanitambua, viwanja hivyo ni vya ukoo nikienda kuomba nakala hawataki kunipatia na aliyeninyima hizo nakala ni Catres,"alidai mwananchi huyo.

Makonda alisema kuna tabia ya baadhi ya watendaji wa ardhi huchukua maeneo ya watu wanapoyapima.

"Kwa kigezo cha kusema sheria sheria katika hili hapana. Sheria inamtambua mwenye ardhi, Mkuu wa Wilaya kaa na huyo mama kabla sijashuka hapa mniambie hivyo viwanja vinne vipo kwa nani?,"alihoji.

Makonda alimuagiza Mkuu wa Mkoa Kagera, Fatma Mwasa, kutenga muda kwa ajili ya kusikiliza kero za ardhi na atakuwa anafuatilia suala hilo ili wananchi wapate haki zao.

"Rais Samia ni zao la wote asitokee mtu akapita huku Kanda ya Ziwa akasema mnabaguliwa hapana. CCM ni chama bora cha siasa na chenye misingi bora, mimi ni zao la John Magufuli amenichukua ukisikia mtu anasema huku kanda tunabaguliwa mwambie, 'mbona Makonda yupo," alisema Makonda.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Stella Kahwa akikabidhi cheti mmoja wa wanafunzi bora wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), wakati wa kongamano chuoni hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# CBE sasa kufundisha kozi kidijitali

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimesema kuanzia mwakani kitaanza kufundisha baadhi ya kozi kwa njia ya mtandao ili kuwawezesha watu wengi kusoma masomo ya biashara.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, alisema hayo juzi wakati wa kongamano kueleekea mahafali ya 58 ya chuo hicho yaliyofanyika jana Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

Alisema, CBE imekuwa ikishirikiana na taasisi mbalimbali kutoa wahitimu bora zaidi na wameshatia saini mkataba na Wakala wa Vipimo (WMA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Elimu Mtandao (eGovernment) kwa ajili ya kuendesha program za uanagenzi na atamizi.

"Sasa hivi tumeona elimu tunayotoa tuiboreshe zaidi. Kwa hiyo tunatarajia baada ya hiyo mikataba kutiwa Saini, kuanzia mwakani tutaanza kutoa mafunzo ya metrolojia kwa vitendo zaidi ambayo yanakuwa ya uanagenzi kwa wanafunzi wetu kusoma na kwenda kufanya kazi kwa vitendo," alisema.

Pamoja na kuboresha uhusiano na vyuo na taasisi za ndani ya nchi, alisema CBE imeendelea kuimarisha uhusiano na vyuo vya nje ya nchi na kwa sasa wafanyakazi wanane wa chuo hicho wanasoma shahada za uzamivu (PhD) nchini China kwenye uchumi na uhasibu. Pia alisema, chuo hicho kina uhusiano mzuri na Chuo Kikuu cha Eastern cha Finland ambako wamekuwa wakizalisha wataalamu wa fani ya biashara na walimu watano wameshahitimu ngazi ya PhD na wengine wanaendelea na masomo yao.

Alisema katika kuboresha utafiti wa chuo hicho na taaluma, chuo kimeendelea kufanya makongamano kujadili masuala mbalimbali kila mwaka na mwaka huu kongamano hilo litafanyika mkoani Dodoma.

Alisema CBE imekuwa ikiboresha mitaala na katika kipindi cha miaka mitano wamefanikiwa kuingiza sokoni program 10 kuanzia ngazi ya Stashahada mpaka Shahada ya kwanza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Stella Kahwa, alisema kwa sasa nchi inahitaji vijana wabunifu watakaoweza kuziweka nadharia za darasani katika vitendo.

"Nimetembelea maonyesho yenu nimeona ubunifu mbalimbali wa wanafunzi na hata wajasiriamali ambao wamepitia program atamizi wameweza kufungasha bidhaa zao kitaalam sana mpaka nimeshangaa na zimefikia viwango vya kimataifa," alisema

Alikipongeza chuo hicho kwa kuanzisha progamu atamizi na ya uanagenzi ambayo imewezesha wanafunzi kusoma kwa vitendo na kuvunja mipaka ya nadharia kwa kufanya miradi ya utafiti kwa vitendo.

# Mjadala wa ufisadi bungeni ni faida ya uwazi wa Rais Samia

**Na Kambi Mbwana**

IMEKUWA kawaida sasa kuona watu mbalimbali, wakiwemo wanasiasa, wanauchumi na baadhi ya viongozi wa dini, wakisimama hadharani kutoa maoni yao bila woga, wakitumia haki ya katiba, Ibara ya 18.

Kama hiyo haitoshi, ndani ya Bunge, wimbo ni namna gani ndani ya halmashauri nchini kumeibuka mchwa wanaofuja mabilioni ya fedha na kusababishia hasara serikali na wananchi wake kuendelea kupata shida.

Ndani ya Bunge, wabunge wengi walipata nafasi ya kuchangia, katika mkutano uliotamatika jana, kwa mfano, walisimama kidete kupigia kelele suala hili, wakisema suala hilo linakwamisha juhudi za serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa akihangaika kutunisha mfuko wa serikali kwa kuimarisha vyanzo na mawanda mapana ya kiuchumi.

Hoja na mijadala ya wabunge, imekuja wakati mwafaka kwa kuwa wanayo haki na mamlaka ya kuchangia kwa faida ya nchi ya Watanzania.

Wao ndio wanaoendesha chombo kinachoisimamia serikali, hivyo uwapo wao bungeni una faida kubwa kwa nchi.

Katika kuangalia jambo hili linalozua utata, shukrani ziende kwa Rais Samia. Uwazi na misingi ya kidemokrasia anayoiendeleza ina faida kubwa.

Maoni ya namna yoyote hata kama ni mabaya kwa serikali, yanatokana na uwazi wake anaosisitizwa mara kwa mara ni Rais Samia ndiye aliyeruhusu pia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye kazi yake kwa uwazi bila kuingiliwa na muhimili wowote.

Ofisi hiyo ya CAG sasa inafanya kazi zake kwa uhuru bila kuhofia matokeo ya taarifa zake inazotoa mbele ya umma.

CAG ameupata uhuru huo zaidi katika serikali ya ya sasa chini ya Rais Samia pamoja na kumwongezea bajeti ili afanye kazi kwa ufanisi.

Hali hiyo haikuwapo katika awamu iliyopita, kwa kuwa uhuru huo haukutolewa ili kutoa maoni ovu dhidi ya serikali bali ilishuhudiwa sifa tu zikitamalaki kila eneo. Hakukuwa na mtu aliyekuwa huru kukosoa serikali.

Mtu aliyefanya hivyo, alikutana na rungu la serikali jambo lililoibua woga ndani ya jamii. Ni wakati ambao wanasiasa wa upinzani walinyamazishwa.

Hata vyombo vya habari navyo vilikutana na shughuli pevu.

Mwaka 2018, CAG wa wakati huo, Prof. Mussa Assad, aliingia kwenye mzozo mzito na serikali kiasi cha kupoteza kazi. Chanzo kilianza baada ya kutoa ripoti ya ukaguzi na kuonyesha Sh, trilioni 1.5 hazijulikani zilikwenda wapi.

Hiyo ilikuwa ripoti ya bajeti ya mwaka 2016/2017 ambayo ilikuwa ya kwanza kwenye serikali ya awamu ya tano chini ya Hayati John Magufuli.

Aliyekuwa Mbunge wa Kigoma Mjini kupitia ACT - Wazalendo, Zitto Kabwe, alikuwa mmoja wa wanasiasa wa upinzani waliohoji matumizi ya fedha hizo.

Taarifa ya hesabu ya Mfuko Mkuu wa Serikali ilionyesha makusanyo ni Sh. Trilioni 25.3 lakini baadaye matumizi yakawa Sh Trilioni 23.79 na kuibua mjadala mzito.

Prof. Assad hakusema kama fedha hizo zimeibiwa bali alionyesha wasiwasi wa matumizi yake kwa kuwa hadi anakamilisha ripoti yake hayakujulikana.



Rais Samia Suluhu Hassan.



Spika Dk. Tulia Ackson.

Hoja hii ilipokewa kwa ugumu na serikali. Kuonyesha Bunge nalo lilifanya kazi kwa kusikiliza matakwa ya uongozi wa serikali, likaanzisha mchakato wa kumtaka Prof. Assad ajieleze kwao huku likitaka awaombe radhi.

Prof. Assad aliitwa Bungeni Januari 21, 2018 na Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa madai kuwa walidhihakiwa kwa kuitwa 'Bunge Dhaifu', wakati anajenga hoja yake ya upotevu wa Sh. trilioni 1.5.

Hoja ya udhaifu wa Bunge la wakati wa Spika Job Ndugai huenda ilikuwa inafanana na ukweli kwa sababu si tu lilimuita Assad ajieleze, bali pia ilishuhudiwa akitimuliwa kazi bila kufuata utaratibu.

Kama wabunge walikuwa wanajua wajibu wao, wangepinga kuitwa dhaifu kwa vitendo kwa kuhakikisha wanapata majibu sahihi ya fedha za serikali zilizokuwa zinapiganiwa na ofisi ya CAG.

Walinyamaza kimya wakipotezea hoja ya upotevu huo lakini pia wakipambana wasafishwe baada ya kuitwa dhaifu na CAG.

Bunge lisipokuwa dhaifu linaweza kuwa na faida kubwa kwa taifa kwa sababu litasimamia vizuri serikali kwa mambo mbalimbali yakiwamo ya fedha za umma. Kwa mfano Mei, 2014, kashfa ya ufisadi katika akaunti ya Tegeta Escrow iliibuliwa bungeni na iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

Akaunti hii ilifunguliwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa lengo la kuhifadhi fedha za malipo ya tozo ya ufuaji umeme baada ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuingia kwenye mgogoro na Kampuni ya IPTL na suala hilo kutinga mahakamani.

Katika kashfa hiyo iliyotikisa katika serikali ya awamu ya nne chini ya Rais Jakaya Kikwete huku Spika wa Bunge akiwa Anne Makinda, ilishuhudiwa mvutano mkubwa wa wabunge wakisimama kidete kuchangia ili kupata undani wake.

Wabunge kama Deo Filikunjombe (sasa marehemu), David Kafulila na Zitto Kabwe walisimama kwa upande wa haki huku bunge nalo likisimama katikati kusikiliza na kupokea majibu ya serikali kwa mawanda mapana.

Yanayoendelea sasa ni faida ya uwazi na serikali inayojiendesha kwa misingi ya kidemokrasia. Hali hiyo imesababisha bunge kuonekana imara chini ya Spika Dk. Tulia Ackson. Yote hiyo ni kutokana na falsafa ya Rais Samia.

Si mara moja Rais Samia amesimamia misingi hiyo.

Akiwa jijini Arusha Novemba 24, 2022 wakati akifungua Mkutano wa 27 wa mwaka wa Chama cha Wanasheria Afrika Mashariki (EALS), alitumia muda mwingi kuonyesha alivyokusudia kuongoza taifa linalojipambanua kwa haki, uwazi, demokrasia na utawala bora.

"Ndiyo maana kipindi hiki tumekuja na R nne, Reconciliation, Resilience, Reform and Rebuilding na tumeshaanza na 'reconciliation' miongoni mwetu, ndiyo maana mnasikia Tanzania imekaa vizuri," alisema.

Akichangia hoja ya mjadala wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na PAC, Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Musukuma, alionyesha hofu kubwa ya kinachoendelea serikalini, huku akitaka watu wanaotajwa kwenye ufisadi wachukuliwe hatua.

Taarifa ya LAAC ukurasa wa 91 inasema kuna ukiukwaji wa sheria ya ununuzi wa umma na kusababisha upotevu wa Sh. bilioni 106.799, huku PAC yenyewe, ukurasa wa 147, ikisema serikali inatumia Sh. bilioni 5.7 kwa mwaka kugharamia chakula cha wafungwa 3,000 waliomaliza adhabu zao.

Kwa kusimama hadharani kuzungumzia hali inavyoendelea kwenye jamii bila kusahau kuanika vitendo vya kifisadi vinavyofanywa na baadhi ya watumishi serikalini, taifa linaelekea kuzuri.

Sababu kubwa ni kwamba si wote wanaojiliwa serikalini ni waaminifu. Wako kwenye nyadhfa kwa sababu wanazojua na hawana uchungu na taifa.

Wako kwa maslahi binafsi, hivyo si vibaya kuweka wazi vitendo vichafu kama ilivyo dira ya Rais Samia.

Kinachofanyika sasa ni kuendesha serikali kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa sambamba na kujiridhisha kabla ya kuchukua hatua.

Mfano ni sakata la watumishi mkoani Mtwara waliotumbuliwa kutokana na kauli ya Rais alipokuwa ziarani mkoani humo Septemba 16, mwaka huu.

**kambimbwana@gmail.com**
**0712 053949**



## Vichanga Krismas 'kulamba' bingo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Vodacom imezindua kampeni yake ya 'Sambaza Shangwe, Gusa Maisha' kwa lengo la kutoa bima ya afya kwa mama na mtoto Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar na kuwapa wateja wake zawadi, wakiwemo watoto wachanga watakaozaliwa wakati wa Krismas na mama zao.

Akizungumza katika uzinduzi huo jana, Mkurugenzi wa Biashara na Masoko wa Vodacom Tanzania, Linda Riwa, alisema kuwa msimu huu wa sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya wa 2024 utakuwa wa kipekee kwa kuendesha promosheni zinazolenga kuwazawadia wateja wao.

Riwa alisema katika kipindi hicho, Vodacom Tanzania, watatoa bima ya afya kwa watoto watakaozaliwa Desemba mwaka huu na mama zao.

"Sambaza Shangwe, Gusa Maisha - kama jina la kampeni linavyojieleza, inalenga kusambaza shangwe na kugusa maisha ya wateja wetu nchini kote," alisema na kuongeza kuwa:

"Tutahakikisha wateja wanabakia na tabasamu na kuwa katika hali ya shamrashamra tunapoelekea kufunga mwaka, tutaendesha droo za wiki, wateja wenye bahati watajishindia zawadi za pesa taslimu mpaka kiasi cha Shilingi milioni 10, bodaboda, luninga, simu janja, routers za 5G na 4G na nyinginezo nyingi."

'Sambaza Shangwe, Gusa Maisha' inatarajiwa kudumu kwa takribani wiki 10 mpaka katikati ya Januari mwakani.

Kwa mwezi huu, alisema itawazawadia na kuwakabidhi wateja zawadi mbalimbali na Desemba zawadi ya upendo ya bima kubwa ya afya kwa mama na mtoto.

Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, alisema Vodacom inatambua kuwa katika msimu wa sikukuu hizo za mwishoni mwa mwaka, Watanzania wengi hufanya manunuzi na malipo ya huduma, hivyo inawahimiza kufanya miamala kwa M-Pesa kwa kuwa ni njia rahisi na salama zaidi kwa fedha zao.

## Serikali yajipanga kudhibiti magonjwa ya milipuko nchini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI inaendelea kufanya tathimini ya kukabiliana na magonjwa ya milipuko kwa kuboresha maeneo yanayolinda afya za wananchi nchini, imeelezwa.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi wakati wa kikao kazi cha makatibu wakuu nchini kupitia na kujadili rasimu ya taarifa ya tathmini ya hali ya utekelezaji wa afya kwa wote na utayari wa kukabiliana na dharura kilichofanyika jijini hapa.

Kwa mujibu wa Dk. Yonazi, kuna umuhimu wa kufanya tafiti na tathmini hizo kwa kuzingatia uwepo wa milipuko ya magonjwa kwa kuboresha maeneo yanayolinda afya za watu.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, alisema wanaendelea kujipanga ili kuhakikisha wizara hiyo inadhibiti na kukabiliana na magonjwa hayo na huduma za afya zinapatikana wakati wote nchini.

# Biteko: Gesi kuchochea uchumi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amesema kuanza kwa ujenzi wa mradi wa bomba la kusafirisha gesi kati ya Tanzania na Uganda kutachochea uchumi na kuimarisha sekta ya nishati.

Katika upembuzi utakaofanyika kwa mwaka mmoja kwa ushirikiano ni asilimia 50 kila nchi itanufaika na mradi huo wa gesi asilia kutoka Tanzania kwenda Uganda.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini wa mkataba wa kusafirisha gesi hiyo, Biteko, alisema hatua hiyo itafikiwa baada ya kuanza kwa kazi ya upembuzi yakinifu wa mradi huo.

Alisema upembuzi huo utawezesha kufahamu tathmini ya mradi na kutoa mwongozo wa uwezekano ikiwamo muundo wa mradi, mahitaji ya gesi, ukubwa wa bomba na taarifa nyingine muhimu kwa ajili ya kufanya uamuzi.

"Nishati ni ufunguo wa maendeleo kwa nchi yoyote ile duniani na umoja ni nguvu, natoa wito kwa nchi hizi mbili kutumia fursa ya kutekeleza mradi huu ambao utaunganisha katika nyanja ya kiuchumi na kijamii," alisema.

Alibainisha kuwa licha ya Tanzania kugundua kiasi kikubwa cha gesi asilia takribani futi za ujazo trilioni 57.54, mahitaji ya rasilimali hiyo yanaongezeka kwa kasi ndani na nje ya nchi.

Alisema Tanzania inazalisha mita za ujazo milioni 250, hadi sasa asilimia 80 ya gesi inatumika kuzalisha umeme na 20 zinazobaki kwa ajili ya viwandani, nyumbani na usafirishaji.

"Hii inafanya serikali kuweka nguvu zaidi katika utafutaji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa nishati hiyo katika maeneo yakiwemo Eyasi Wembere, Mnazi Bay Kaskazini, Songosongo Magharibi, Ziwa Tanganyika na katika kina kirefu cha maji baharini," alisema.

Dk. Biteko alisema kutiwa saini kwa mkataba huo kumetokana na makubaliano ya awali yaliyosainiwa Agosti, mwaka 2018 kwa ajili ya ujenzi wa bomba hilo kutokana na Tanzania kugundua kiasi kikubwa cha gesi katika kina kirefu cha bahari na nchi kavu.

"Tanzania inaendelea kutafuta wabia wa kimkakati watakaoweza kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ili kutafiti na kuendeleza vyanzo vya upatikanaji wa mafuta na gesi," alisema Biteko ambaye pia ni Waziri wa Nishati.

Waziri wa Nishati na Maendeleo ya Madini wa Uganda, Ruth Nankabirwa, alisema nchi yake inatambua umuhimu wa mradi huo na kumekuwepo na mahitaji makubwa ya matumizi ya gesi, hivyo wana kila sababu ya kuhakikisha kunakuwepo na uharakishwaji wa mradi huo.

Aliziomba taasisi za kimataifa zinazotoa fedha zenye masharti nafuu kuja kuwekeza katika mradi huo ambao ni kitambulisho nchi za Afrika Mashariki zinaweza kuendesha miradi inayohusu mageuzi katika sekta ya nishati.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Maendeleo ya Madini ya Uganda, Irene Batebe, alisema upembuzi wa mradi huo, utaanza mwaka wa fedha 2024/25 na kuzitaka nchi wanachama kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo muhimu kwa uchumi wa nchi hizo mbili.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akionyesha tuzo baada ya kukabidhiwa na Bodi ya Usajili wa Wathamini, baada ya kufungua Mkutano Mkuu wa Nne wa Bodi hiyo, jijini Dodoma juzi, ikiwa ni pongezi za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa juhudi zake za kuwaletea maendeleo Watanzania na kuwajengea uwezo wa kujitegemea. Kushoto ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda. **PICHA: OWM**

# Upungufu wa umeme bado pasua kichwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, ametaja hatua zinazochukuliwa na Serikali kukabiliana na upungufu wa umeme nchini.

Akizundua Jukwaa la 13 lililoandaliwa na Taasisi ya HakiRasilimali, Kapinga alisema Serikali imeendelea kujiimarisha kwa kuwekeza kwenye vyanzo vya uzalishaji umeme ikiwamo gesi asilia ili kumaliza tatizo la upungufu wa nishati hiyo nchini.

"Tumeongeza uzalishaji kwenye visima vyetu vya Songosongo na Madiba ili kuongeza gesi na kupunguza changamoto ya upatikanaji wa umeme na tunafanya maendeleo kwenye mitambo yetu yote ili hali ya upatikanaji wa umeme iendelee kutengamaa," alisema.

Aliongeza kuwa: "Tunathamini mchango mkubwa wa asasi za kiraia katika masuala ambayo yanahusu maendeleo ya Watanzania na wizara vyanzo vyetu ya kuzalisha umeme vinahusiana na sekta ya uziduaji husan sekta ya gesi."

Alisema jukwaa hilo litasaidia Serikali kuona namna ya kuwekeza zaidi kwenye vyanzo rafiki kwa mazingira ya uzalishaji umeme nchini.

Naibu Waziri huyo aliwapongeza HakiRasilimali kwa kuandaa jukwaa hilo kujadiliana namna ya kutumia rasilimali kwa maendeleo na utunzaji wa mazingira nchini.

Mkurugenzi wa HakiRasirimali, Adam Antony, alisema wameandaa jukwaa hilo ili kuwakutanisha wadau wa uziduaji kujadili jinsi ya kukuza sekta hiyo na kuimarisha sera na sheria za sekta ya uziduaji kwa maendeleo endelevu, ukuaji wa uchumi wa nchi na kuongeza pato la taifa.

Antony alisema vilevile watajadili mazingira rafiki ya uwekezaji, haki za binadamu,uwazi wa mikataba, utoaji leseni, ushiriki wa wanawake na nafasi ya wachimbaji wadogo katika sekta ya uziduaji.

Awali, Askofu Mkuu wa Kanisa la Mennonite Tanzania, Nelson Kisari, alisema sekta ya uziduaji ina faida kwa kukuza uchumi wa nchi na kushauri Serikali kutunga sera na miongozo kulinda rasilimali za nchi na kuwanufaisha Watanzania.





# Benki yapiga jeki ujenzi hospitali

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imetiliana saini mkopo wa dola milioni 163.6 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani Binguni na Benki ya Exim ya nchini Korea Kusini.

Akizungumza jana katika hafla iliyofanyika Ofisi za Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Amina Khamis Shaaban, alisema mradi huo ni kipaumbele cha SMZ.

Alisema baada ya SMZ kuona umuhimu huo waliomba mkopo huo kwa Korea kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo ili kuondokana na gharama za kupeleka wagonjwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na nchini India kwa matibabu zaidi.

"Mradi huu ni muhimu kwa Serikali ya Zanzibar na Tanzania na tukifanikiwa naamini tatizo la kupeleka wagonjwa nje ya nchi litapungua na wataalamu wa sekta ya afya kupata eneo la kusomeshea kwa vitendo," alisema.

Dk. Marijani Msafiri, Mkurugenzi wa Tiba Wizara ya Afya Zanzibar, alisema mradi huo ambao ni muhimu kwa Zanzibar na Hospitali ya Rufaa Mnazimmoja pamoja na kufanyiwa ukarabati mkubwa, haiwezi kuweka huduma zote za kibingwa.

Alisema tatizo kubwa lililokuwepo Wizara ya Afya Zanzibar ni gharama kubwa inayotumika kusafirisha wagonjwa nje ya nchi.

"Tuna mikataba na hospitali tatu za Taifa Muhimbili ikiwemo Muhimbili yenyewe, Taasisi ya Mifupa (MOI) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, tunalipa fedha nyingi kuwapeleka na wagonjwa wanaoshindikaza India kwani tungeweza kufanya matibabu kwa wagonjwa hawa kama tungekuwa na miundombinu na majengo ya kisasa hapa Zanzibar," alisema.

Dk. Marijani alisema ujenzi wa hospitalui hiyo utaongeza idadi ya wataalamu wa afya kujifunza kwa vitendo.

Alisema hospitali hiyo itakuwa na huduma za kibobezi za kisasa za upasuaji wa uti wa mgongo, ubongo, moyo, kupandikiza figo na matibabu ya magonjwa ya watoto.

Naibu Waziri huyo, alisema wizara hiyo itaendelea kusaini mikataba na kutafuta mkandarasi wa ujenzi wa hospitali hiyo mwakani.

# Wataalamu wazawa kufanya utafiti mafuta, gesi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesema kuna haja ya kutumia taasisi za Tanzania Bara kufanya utafiti wa nishati ya mafuta na gesi visiwani hapa ili kukuza pato la taifa, kukuza uchumi na kuondokana na gharama kwa kutumia wataalamu wa nje.

Hayo yamo katika hotuba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, iliyosomwa juzi na Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduwara, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wanachama wa Jumuiya ya Wajiolojia Tanzania (TGS) unaofanyika visiwani hapa.

Dk Mwinyi alisema ni muhimu kutumia wataalamu wa ndani ya nchi kufanya utafiti wa rasilimali zilizoko nchini zikiwamo mafuta, gesi na maji kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kubadilishana uzoefu wa kazi na kupunguza gharama kwa kutumia wataalamu wa nje ya nchi.

Alisema SMZ inatarajia kuzitumia taasisi za Muungano kwa sababu zimepiga hatua kubwa katika utafiti wa rasilimali hizo.

Alisema malengo ya serikali yake ifikapo mwaka 2025 ni kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama unaongezeka hadi kufikia asilimia 85 kwa wananchi wake.

Rais Mwinyi aliitaka Mamlaka ya Majisafi na Salama Zanzibar (ZAWA) kufanya kazi na wataalamu wa jumuiya hiyo ya utafiti wa rasilimali ya maji safi na salama ili kufikia malengo ya kusambaza huduma hiyo kikamilifu kwa wananchi wakiwemo wa vijijini visiwani hapa.

Rais wa Jumuiya hiyo, Dk. Elisante Mshiu, alisema timu ya wataalamu wa Wajiolojia Tanzania Bara inatarajiwa kuwasili Zanzibar kutayarisha ramani ya viashiria vya utafiti wa rasilimali asilia zilizopo visiwani hapa.

Dk. Mshiu aliwataka wanafunzi wa kike kujiunga na elimu ya juu katika fani ya jiolojia ili kukabiliana na ushindani katika soko la ajira duniani katika utafiti wa rasilimali asilia.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano kuna mafanikio makubwa kwa wanafunzi wengi wa kike kujitokeza na kujiunga na taaluma hiyo, ikiwemo utafiti wa rasilimali ya mafuta, gesi na madini.

Mhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) katika shahada ya kwanza ya mafuta na gesi, Aziza Amour Juma, aliwataka wasichana wanaomaliza kidato cha nne na sita kujiunga masomo ya jiolojia ya sayansi elimu ya juu kuhusiana na tafiti za rasilimali za taifa. Aziza alisema kuna imani potofu imejengeka katika jamii kuwa masomo ya sayansi katika fani ya jiolojia ni kwa ajili ya wanaume kutokana na ugumu wake na utafiti.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Washauri wa Wajiolojia nchini, Profesa Abdulkareem Mruma, aliwataka wataalamu nchini kufanya kazi za utafiti na kuleta matumaini katika jamii.

Mkutano huo unaofanyika kila mwaka, umehudhuriwa na wataalamu 300 wakiwemo wanafunzi wa taaluma hiyo UDSM ambao wamesisitiza umuhimu wa kufanyika tafiti na kuimarisha uchumi nchini.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Reliance Insurance Co. Ltd, Ravi Shankar (kulia), akijadiliana jambo na Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Baghayo Saqware (katikati) na Mwenyekiti wa Bodi ya Reliance, Leonard Mususa wakati wa kuadhimisha miaka 25 ya kampuni hiyo na ufunguzi wa Ofisi mpya ya makao makuu eneo la Victoria, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# EU yajitosa uchumi wa buluu Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UMOJA wa Ulaya (EU) umeahidi kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kufanikisha mradi wake wa uchumi wa buluu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu, Aboud Suleiman Jumbe, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya ujumbe wa EU kumaliza ziara katika Kituo cha Kuhifadhia Samaki kilichoko Malindi Unguja, Kiwanda cha Kusarifu Dagaa Kamba na Fungu Refu. Alisema kupitia mradi huo kuna fursa watapata, ikiwemo misaada na mkopo nafuu wa fedha kutoka benki.

Alisema wizara yake na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania wanaishukuru EU na kuahidi kushirikiana kwenye sekta ya uvuvi wa bahari kuu, uchumi wa buluu, elimu, teknolojia na uimarishaji wa mifumo ya biashara ya baharini. Awali, ujumbe huo ulikutana ofisini kuzungumzia programu za umoja huo, uchumi wa buluu Zanzibar, miradi ya uimarishaji wananchi na ushirikiano.

Pia alisema walizungumzia kuhusu umoja huo kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika sera, mipango na sekta ya uvuvi Bahari ya Hindi na maeneo ya nje ya mipaka ya kimataifa na sekta mpya ya uvunaji wa madini na mazao ya Bahari.

Mkurugenzi Mkuu wa Kamisheni ya Uvuvi na Bahari wa EU, Charlina Vitcheva, alisema jumuiya hiyo iko tayari kushirikiana na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) katika uchumi wa buluu na uvuvi mdogo wa bahari kuu.



TUPAC UKURASA 14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI NOVEMBA 11, 2023



# WAMEYATIMBA VIBAYA

WANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Whozu, Billnass na Mbosso hivi karibuni wamejikuta wakipata kibano kikali baada ya kufanya ukaidi na kutoa video yenye ukakasi kwa jamii.

Baraza la Sanaa Tanzania (Basata) licha ya kuwatoza faini ya shilingi mil 3 kila mmoja, pia limewafungia kutojihusisha na kazi za muziki kwa kipindi cha miezi mitatu.

Kilichofanywa na wanamuziki hao ndani ya wimbo huo unaoitwa 'Ameyatimba' ni wazi hayakubaliki kutokana na kuonyeshwa vitendo ambavyo havipaswi kuonekana hadharani.

Baadhi ya wadau wamesema kwamba Whozu ambaye ndiye mwenye wimbo huo ameshindwa kujitambua kama yeye nani na kutoa video ambayo hata yeye mwenyewe akiitazama hawezi kuimaliza kutokana na ukakasi wake.

Juma Ali amesema wasanii wa Tanzania hawana ubunifu wa kutosha na badala yake wanakimbilia katika vitu vinayoonekana viko kinyume na maadili kama njia ya kupata umaarufu.

"Wakati wa kutengeneza video kila mtu alikuwa akijua hadithi yake, yaani yale yanayoonekana ni kweli waliyaafiki au walitaka kupata umaarufu huku wakijua picha zile ni mbaya? Alihoji.

Celine Mdoe amesema adhabu iliyotolewa sio kali kuliko kitendo ambacho wasanii hao wamekifanya na kuiomba serikali kuongeza ukali ili wasanii waliotaka kufanya kazi kama hiyo kuacha.

Inaelezwa wasanii hao watatu walitumia muda mchache kurekodi wimbo huo wiki iliyopita na kufanya remix ya wimbo huo ambao sasa umekuwa gumzo.

BASI SAWA

## Cecy awataja wanaojua kutupia



MWANAMITINDO maarufu nchini Cecy amewataja wasanii watatu wa Bongo Fleva ambao wanaongoza kwa kutupia nguo kali.

Cecy amewataja wanamuziki hao kuwa ni Ommy Dimpoz, Jux na Diamond Platnumz akiwaelezea ni wanaume wanaopendeza kwa kila nguo wanazovaa.

"Kuvaa ni ubunifu wa mtu na ukifanikiwa kuwavutia watu kwa kila unachokivaa basi utakuwa ni mmoja wa watu wanaopendeza. Wasanii hawa wameweza kuwateka watu kutokana na nguo wanazovaa," amesema Cecy.

## Baba Levo usimponze Diamond

MCHEKESHAJI na mwanamuziki wa kizazi kipya, Baba Levo amesema bosi wake Diamond Platnumz ana fedha za kuwekeza katika timu ya Simba, lakini anahofia kupata matatizo ya kiafya.

Amesema Diamond akichukua jukumu hilo kuna wakati atashindwa kuandika mashairi kutokana na mashinikizo ya mashabiki.

"Diamond ana uwezo wa kuwekeza Simba kwa sababu pesa anazo, lakini siwezi kumshauri kufanya hivyo kutokana na tabia za mashabiki kushinikiza kwa kila kitu," amesema Baba Levo.





## NANDY FEDHA KWAKE SIO KITU

WASANII wa muziki wa kizazi kipya wanazidi kushindana kifedha na sasa wanapishana katika viwanja vya ndege wakiwa na ndege zao maalumu.

Hivi karibuni alikuwa Diamond ambaye alikodi ndege kwa ajili ya kufurahia maisha na familia yake, lakini sasa ni Nandy ambaye ameonyesha jeuri ya fedha kwa kukodi ndege maalum kwa ajili ya kwenda kusherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Ndege hiyo yenye umbo kama gari ndogo ilipambwa kwa vitambaa maalum vilivyoandikwa jina lake na maneno ya kumtakia heri ya kuzaliwa yaliambatana na ujumbe wa mwanamuziki huyo akisema yuko njiani kuelekea sehemu kunakofanyika sherehe hiyo.





## Harmonize kuja na Albam kama Serengeti

MWANAMUZIKI mkali wa Bongo Fleva, Harmonize ameitaja albamu yake mpya itakayotoka Novemba 24, sawa na mbuga ya wanyama ya Serengeti ambayo ina wanyama wa kipekee duniani.

Amesema ndani ya Albam ni sawa na mbuga hiyo kutokana na kuwa na nyimbo nyingi tofauti ambazo zitamfanya kila Mtanzania kufurahia.

"Ndani kuna ladha nyingi kama vile wanyama wa Serengeti, ninachowaahidi kila mtu atapata ladha ya muziki anaoupenda ikiwamo Amapiano, Zouk, bolingo na hata muziki wa pwani," amesema.

## WALIOFARIKI NA KUZIKWA UGENINI

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA ya muziki wa Tanzania inaonyesha kuwa mwanamuziki maarufu nchini Tanzania, Mbaraka Mwinsheshe aliyekuwa akipigia bendi ya Moro Jazz na baadaye kuanzisha bendi ya Super Volcano, alifariki dunia Januari 12 1979, Mombasa nchini Kenya.

Huyu anaingia kwenye orodha ya wanamuziki wa Kitanzania waliofariki dunia nchini Kenya, lakini ndiye pekee aliyerejeshwa na kuzikwa Tanzania, kijiji cha Mzenga, mkoani Pwani ambako ndiyo kwao kiasili.

Leo tunawazungumzia wanamuziki wa Kitanzania waliokwenda nchini Kenya kutafuta maisha, lakini kwa bahati mbaya umauti uliwafika huko na mbaya zaidi hawakupata bahati ya kurejeshwa kwenye ardhi ya mama na babu zao, badala yake kuzikwa huko huko ughaibuni kwa sababu mbalimbali.

**George Peter**

Ni mwimbaji, mtunzi, na mpiga magitaa yote ya solo, rhythm na bass. George na kaka yake Willson Peter Kinyonga waliibukia Hale mkoani Tanga kwenye bendi ya Jamhuri Jazz Band mwishoni mwa miaka ya '60 na mwanzoni mwa miaka ya '70. Walijiengua na kwenda kuunda Arusha Jazz Band iliyoingia nchini Kenya na kubadisha jina kujiita Simba Wanyika.

Aina ya uimbaji wa George ndiyo uliomuathiri TX Moshi William ambaye kwa kiasi kikubwa aliiga uimbaji wake. Alifariki Dunia mwaka 1992 na kuzikwa nchini Kenya.

**Willson Peter Kinyonga**

Ni mtunzi, mwimbaji, mpiga gitaa la solo na kiongozi wa bendi ya Simba Wanyika. Ustaa wake ulianza kwenye bendi ya Jamhuri Jazz band ya Tanga, kabla ya kuunda Arusha Jazz Band na wenzake wakaingia nchini Kenya.

Akiwa na ndugu yake George waliiletea heshima kubwa Tanzania kutokana na nyimbo zao zilizopendwa na kuvuma Afrika Mashariki yote. Nyimbo kama 'Sofia', 'Pamela', 'Polepole', 'Halima', na nyingine nyingi ziliifanya bendi hiyo kupendwa na wengi. Alifariki dunia mwaka 1995 na kuzikwa nchini Kenya.

**John Ngereza**

Wimbo wa 'Afro', ni maarufu sana hapa nchini, ukipigwa na bendi nyingi kwenye kumbi na baa mbalimbali. Lakini wengi hawajui mtunzi wa wimbo huu.

John Ngereza, ndiye mtunzi wa wimbo huu akiwa na Les Wanyika. Ni mmoja wa Watanzania waliokwenda nchini Kenya kutafuta maisha na alifanikiwa kujiunga bendi hiyo.

Ni mwanamuziki maarufu sana nchini Kenya akiwa pia amepitia bendi mbalimbali za huko.

Alifariki dunia mwaka 2002 na kuzikwa nchini Kenya.

**Profesa Omari Shaaban**

Ukizisikiliza nyimbo za Simba Wanyika na Les Wanyika, kuna wakati gita la 'rhythm' linaachiwa na linasikika peke yake, likisindikizwa na drums, huku kuna sauti ikisikika 'Profesaaa Omari'.

Mtu huyo alikuwa mpiga gita hilo la kati na kuufanya muziki wa Simba Wanyika na Les Wanyika kukubalika sana nchini Kenya.

Awali alikuwa Simba Wanyika, lakini baadaye naye akaenda kujiungua na kwenda kuunda Les Wanyika, wakiwaacha ndugu hao na bendi yao. Alifariki mwaka 1998 na kuzikwa nchini Kenya.

**Twahir Mohamed**

Inasemekana Tanzania haijapata mpuliza saxaphone kama Twahir Mohamed Twahir. Huyu alikuwa na uwezo na pumzi ya kupiga chombo hicho kuanzia mwanzo wa wimbo hadi mwisho.

Hapa nchini alipigia bendi mbalimbali ikiwemo Orchestra Safari Sound (OSS), kabla ya kwenda nchini Kenya kwenye bendi ya Simba Wanyika kuziba pengo la Liza Elias, Mtanzania aliyeamua kurejea nchini na kujiunga na Mwenge Jazz Band wakati huo.

Alipigia bendi mbalimbali nchini Kenya ikiwemo Virunga ya Samba Mapangala, kabla ya kufariki dunia 2004 nchini Kenya na kuzikwa kwenye makaburi ya Kibera.

FILAMU

## Masikini wa Mungu: Mtenda Hutendwa

**Na Adam Fungamwango**

MASIKINI wa Mungu ni filamu iliyojaa mafunzo yenye simanzi, huzuni na masikitiko matupu. Ukiitazama utakuta ukibubujikwa tu na machozi. Ni filamu inayoonyesha baadhi ya binadamu wenye akili na mawazo mabaya kuliko shetani mwenyewe.

Ali Nogi, mmoja wa wazee wa mtaa mmoja hapa nchini ana tabia za uchawi na pia tamaa ya madaraka.

Anamtengenezea mazingira ya kuchukiwa Mwenyekiti wa Serikali iliyopo. Na akachukiwa sana. Haikushangaza hata alipowatuma watu wa kazi ambao anawafuga kwa kazi ya kuua watu, akaenda kummaliza. Hakuna huzuni yoyote iliyokuwa kwenye mtaa huo.

Akamuua kwa njia za kishirikiana na jirani yake Nico, aliyehofia kuwa anaweza kuchukua madaraka.

Kifo cha Nico na mkewe kilichotokana na kuuawa kwa njia za kishirikina kilikuwa pigo kwa watoto wawili Kamo na kaka yake ambao waliachwa bado wadogo.

Walikuwa wakisaidia chakula na mama wa nyumba ya jirani. Hata hivyo, pamoja kuishi maisha ya taabu, lakini bado mze Ali Nogi na kundi lake la watesaji na wauaji walikuwa wakiifuatilia na kuwasumbua watoto wa marehemu ili wasipate utulivu na kuamua kulipiza kisasi mbele ya safari.

Hilo linafanikiwa baada ya mzee huyo kumfanya kaka wa Kamo kupooza.


Katika pitapita yake, Kamo anamkuta anamsaidia mwanamke mmoja mtaani aliyevamiwa na vibaka baada ya kumgonga mtu na gari.

Mwanadada huyo, Wolper anatokea kumpenda Kamo na kuamua kwenda nyumbani kwake. Anashuhudia yeye na kaka yake wanavyoishi maisha ya kifukara.

Kuwa na demu mkali kama huyo kunawakera wale vijana wahuni wanaotumiwa na Ali Nogi, wanampelekea ushahidi wa uongo Wolper, anambadilikia Kamo na kumuacha. Mkuu wa kundi la mauaji ndiyo anayemchukua.

Kamo anakasirika na kwenda kutaka kulipiza kisasi, lakini anaishia kuwekewa dawa kwenye macho, Hata hivyo, mwanamama anakutana na ukweli usiopingika na ushahidi wa kutosha kuwa aliyokuwa akiambiwa yote si ya ukweli, hivyo akamkimbia mkuu wa kundi, akarejea kwa Kramo.

Akampeleka hospitalini na macho yake yakaanza kuona tena. Waliporudi walimkuta mzee Ali Nogi akiwa kwenye kampeni ya Uenyekiti wa Serikali za Mitaa. Alipowaona alishtuka na ukweli kuhusu tuhuma zake zote zikaanikwa hadharani kwa wananchi siku hiyo.



# Wapenzi wa Tupac bado wanasubiri



MASHABIKI na wapenzi wa rapa maarufu, marehemu Tupak Shakur, itawabidi kusubiri hadi Juni 3 mwakani ili kujua hatma ya kesi iliyofunguliwa dhidi ya mauaji ya msanii huyo.

Kesi inayomkabili Keffe D' Davis ambaye ni kiongozi wa genge la kihalifu, ameshitakiwa kupanga na kufanya mauaji ya Shakur miaka 27 iliyopita.

Davis ndiye mtu pekee aliyekuwa ndani ya gari aliyehusika kufyatua risasi ambayo ilimuondoa uhai rapa huyo wakati akitoka kutazama pambano la ngumi huko Las Vegas nchini Marekani.



## Lori, Damson wamemwagana

PENZI la mwanamitindo maarufu Lori Harvey na mwigizaji Damson Idris limevunjika baada ya kuishi pamoja kwa mwaka mmoja.

Wawili hao walitangaza kutengana kupitia taarifa ya pamoja ambayo walieleza wote wawili wanahitaji kuweka mtazamo wao kamili kwenye njia tofauti.

"Tuko katika hatua ya maisha yetu tofauti, njia zetu zinahitaji umakini wetu kamili na kujitolea. Tunaachana na kubaki marafiki ila upendo na heshima utabaki kwa kila mmoja," imesema taarifa hiyo.

## Reminisce kuitwa baba ni tabu

RAPA maarufu nchini Nigeria, Khalid Safaru, anayefahamika zaidi kama Reminisce, amesema malezi ya watoto yanasababisha yeye na mke wake kuwa katika ushindani wa nani anaonekana anawajali kwa kuwatoa matembezi mara nyingi.

Amesema licha ya umaarufu wake, lakini anajitahidi kuwa baba mwenye bidii kwa kutembea na watoto wake japo si mara nyingi kumpita mkewe.

Amesisitiza kuwa hataki watoto wake wamchukie siku za usoni, hivyo anajitahidi kadiri awezavyo kuhusika katika malezi kwa njia tofauti.





## Naira Marley apata dhamana

SASA ni wazi kwamba mwanamuziki Azeez Fashola, maarufu kama Naira Marley, na msaidizi wake Balogun Eletu, anayejulikana zaidi Sam Larry, wamepewa dhamana ya milioni 20.

Mtandao wa Punch umeripoti kuwa Mahakama ya Yaba, Jimbo la Lagos ilitoa dhamana hiyo kwa mastaa hao ambao wanahusishwa na kifo cha msanii maarufu wa muziki, Mohbad.

Kutokana na dhamana hiyo, Marley na Larry wanatakiwa kusalimisha hati zao za kusafiria za kimataifa ili kuhakikisha kwamba wanasalia nchini humo na pia wanatakiwa kuripoti polisi kila wiki.

## Regina penzi limemkoroga

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Regina Daniels ameweka wazi kwamba yupo tayari kumpatia figo mume wake, Ned Nwoko kuliko baba yake mzazi.

Regina alieleza kuwa ikiwa baba yake na mume wake wote wangekuwa hospitali wana matatizo ya figo, chaguo lake la kwanza ni mumewe Seneta Ned Nwoko kwa ajili ya ustawi wa watoto wake.

Regina Daniels amesema kuwa kuhifadhi afya na maisha ya baba wa watoto wake ni jambo la msingi kwake kama mama.





HABARI KASKAZINI

## Watu 11,000 sasa kupata maji safi

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKAZI 11,000 wilayani hapa Mkoa wa Tanga, wanatarajia kupata maji safi na salama kwa afya zao baada ya kukamilika ujenzi wa mradi wa Tanganyika, Kwemkabala na Masuguru na kuondokana na ukosefu wa huduma hiyo kwa muda mrefu.

Wakazi hao wa kata za Tanganyika, Kwemkabala na Masuguru, wataondokana na adha hiyo baada ya kuunganishiwa maji hadi kwenye makazi yao baada ya ujenzi wa mradi huo kukamilika wakati wowote kuanzia sasa.

Msimamizi wa ujenzi wa mradi huo unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (TANGA-UWASA), Violet Kazumba, alisema ni mwendelezo wa miradi ambayo inajengwa wilayani hapa kwa fedha za Serikali.

Kazumba, alikuwa akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi huo kwa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, walipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa mradi huo na mingine ya Sekta ya Afya na Elimu ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020.

"Lengo la huu mradi hapa Muheza mjini ni kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi, tunataka kumaliza tatizo la maji maeneo ya Tanganyika, Kwemkabara na Masuguru ambao wanapata maji kidogo na kwa mgawo," alisema na kuongeza kuwa:

...Mradi unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi milioni 638, na unajengwa kwa force account (mafundi jamii). Hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 80 na baadhi ya wananchi wa maeneo husika wameanza kunufaika na mradi huu kwa kupata huduma ya maji kupitia vilula saba vya kuchotea maji vilivyojengwa na kukarabatiwa katika maeneo mbalimbali."

Mjumbe wa Kamati ya Siasa CCM Mkoa wa Tanga, Omari Ayubu, aliipongeza TANGA-UWASA kwa kazi nzuri inayoendelea kufanya ili kuhakikisha wananchi wa Muheza wanapata maji safi na kuondokana na mgao ambao umedumu kwa muda mrefu.

Ayubu ambaye alimwakilisha Mwenyekiti wa CCM wa mkoa huo, Rajabu Abdallah, alisema miradi waliyokagua ina ubora na kuwaagiza viongozi wa wilaya hiyo kusimamia na kuhakikisha inakamilika kwa wakati kulingana na ilani ya chama chao, chini ya mwenyekiti wao wa taifa, Rais Samia Suluhu.

Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, Mwenyekiti wa Halmashauri, Erasto Mhina, Mkurugenzi Mtendaji, Jumaa Mhina, Katibu wa CCM, Simoni Leng'ese na Mwenyekiti wa chama hicho wilaya, Laick Gugu kwa nyakati tofauti walimshukuru Rais Samia kwa kuipatia wilaya yao zaidi ya Sh.bilioni 10 kutekeleza miradi ya maendeleo.

# Sumu ya nyuki kutibu magonjwa sugu

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

SERIKALI imeamua kuja na mpango mahususi wa uvunaji wa sumu ya nyuki bila ya kumuathiri baada ya kubaini ina uwezo mkubwa wa kutibu magonjwa ya baridi yabisi, saratani na kisukari.

Jana, Mkurugenzi na Mtafiti Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori nchini (TAWIRI), Dk. Wilfred Marealle, alisema kwa sasa taasisi hiyo imenunua vifaa vya kisasa vya uvunaji wa sumu hiyo.

Aidha, alisema pia iko katika mipango ya kukamilisha maabara ya kisasa ya nyuki na itaanza kutoa elimu namna ya kuvuna zao hilo ili kuongeza pato na tija kwa nchi na wafugaji. "Mazao ya nyuki kama maziwa, sumu yake na poleni (chavua), hivi vinadaiwa kutibu magonjwa kama sukari, saratani na baridi yabisi.

"Utafiti wa matibabu haya, siwezi kuzungumzia kwa undani maana wako watafiti wake kama Muhimbili (Hospitali ya Taifa Muhumbili (MNH), NIMR (Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu), Kitengo cha Tiba Asili na wengine wengi," alifafanua Dk. Mareale.

Inaelezwa kuwa katikati ya mkia wa nyuki, kuna majimaji ambayo ni sumu yenyewe, yakikusanywa yana matumizi katika sekta ya afya.

Soko kubwa la sumu hiyo, liko zaidi India, China, Marekani na nchi nyingine ambazo zinatengeneza dawa.

Vilevile inaelezwa kwamba unapovuna sumu hiyo katika mzinga, una uwezo wa kupata gramu moja hadi tano ambayo ni wastani wa gharama ya sumu ya nyuki kwa soko la nje kuanzia Sh. 150,000 hadi Sh. 350,000 kwa gramu moja.

Gharama hizo zinatajwa kwamba zinategemea mimea ambayo nyuki wametumia kwa kuwa wadudu hao wanatofautiana kulingana na mazingira.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Mlingano, wilayani Muheza mkoani Tanga, Dk. Catherine Senkoro (kulia), akisoma taarifa ya ujenzi wa maabara mpya ya utafiti wa afya ya udongo na uzalishaji wa miche ya mkonge kwa Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Tanga, Omari Ayubu (kushoto), alipotembelea na kukagua jengo hilo akiwa katika ziara ya siku mbili ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo wilayani humo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wafugaji 6,000 duniani kutua Arusha

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANASAYANSI, watunga sera na wafugaji nyuki 6,000 kutoka nchi 113 duniani, wanatarajiwa kukutana jijini hapa kujadili changamoto na kubadilishana uzoefu katika sekta ya ufugaji nyuki na mazao yake.

Mkurugenzi na Mtafiti Mkuu wa Kituo cha Utafiti wa Wanyamapori nchini (TAWIRI), Dk. Wilfred Marealle, alisema Tanzania imechaguliwa kuongoza kongamano hilo mwaka 2027 la 50 lililobatizwa jina la 'API MONDIA'.

Dk. Mareale, alisema kongamano hilo litaambatana na fursa lukuki za utalii, biashara na mijadala muhimu ya sekta ya nyuki na mazao yake.

"Kilichosababisha Tanzania kupata fursa hii adhimu ni kutokana na TAWIRI na Wizara ya Maliasili na Utalii, kushiriki tafiti za kisayansi kwa hatua za awali na kupigiwa kura na nchi nyingi zaidi kuliko nyingine.

"Tanzania ilishindana na nchi za Falme za Kiarabu (UAE), na ikashinda kutokana na kuandika kwa umahiri na kitaalamu kwenye kipengele cha umuhimu wa utafiti katika ufugaji nyuki na mazao yake.

"Tunaomba wadau wote wasikose kongamano hili kwa kuwa ni muhimu kutokana na kukutanisha uzoefu ambao utasaidia kuongeza tija na faida kubwa kwenye sekta ya nyuki. Tunawaomba wafugaji nyuki wajipange kutokosa kutokana na umuhimu mkubwa wa kongamano hilo," alisema.

Mkurugenzi huyo aliwataka Watanzania ambao hawana ajira, kutumia sekta ya nyuki na mazao yake, kujiajiri, kuendesha maisha na kukuza pato la nchi. "Uwekezaji kwenye sekta hii ni rahisi, hauhitaji mtaji mkubwa, unaweka mzinga tu sehemu stahiki, nyuki wanatengeneza asali bila gharama ya uwekezaji," alisema. Tanzania ni nchi ya 12 duniani kwa uzalishaji wa asali, na ya pili Afrika, ikiwa na ekari 48.1 milioni za misitu, makundi ya nyuki milioni 9.2, yenye uwezo wa kuzalisha tani 138,000 za asali.

Kwa sasa Tanzania inazalisha tani 30,800, ikitanguliwa na Ethiopia inayozalisha tani 45,000.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# ‘Kanyaboya’, wizi, utapeli uliotikisa Dar enzi hizo

**Na Adam Fungamwango**

KWA sasa watu wakiliongea au kulisimulia suala hili linakuwa kama burudani tu iliyowahi kutikisa huko nyuma. Watu wanahadithiana na kucheka, kila mtu akikumbuka kisa kilichowahi kumtokea.

Lakini wakati huo ilikuwa ni uchungu mkubwa, kilio cha kusaga meno. Kwenye miji mikubwa na sasa Dar es Salaam, miaka ya 1980 katikati ya miaka ya 1990 kulizuka aina fulani ya wizi au utapeli ulifahamika kwa jina la maarufu, ‘kanyaboya.’

Huu ni aina fulani ya utapeli ambao watu waliuziwa matambara, au kabichi lililochongwa vizuri kwa umbile la viatu.

Walengwa wa utapeli huu ni watu ambao walikuwa wanataka kununua vitu ghali kwa bei nafuu. Walengwa wengine ni wale ambao hawako makini na hawajiongezi.

Wengine ni wazembe na wasiokuwa waangalifu au kukubali kila wanachoambiwa bila kutia shaka, lakini pia wapo ambao bado hawakuwa na uelewa, hasa wale waliokuwa wanatoka mikoani.

Jiji la Dar es Salam, hasa maeneo ya Manzese, Ilala, Kinondoni, Kariakoo, maeneo ya Shule ya Uhuru, na maeneo mengine ya biashara aina hii ya utapeli ilishamiri sana.

Cha ajabu ni kwamba, pamoja na kwamba tayari utapeli huu ulikuwa maarufu na kila siku watu walisimuliana jinsi walivyotapeliwa.

Hata badhi ya bendi ziliimba kuwaasa wananchi wawe makini na utapeli wa aina hiyo.

Wimbo ulitwao ‘Mwisho wa Mwezi’ wa Vijana Jazz, una baadhi ya maneno yanayowatahadharisha wananchi kuwa makini na utapeli wa aina hiyo.

“Mwisho wa mwezi ukifika eee, ukifika eee, abiria chunga mfuko wako kakaaa, Mwananyamala Posta eee, Manzese, Kariakoo, Tandika Shule ya Uhuru kaka eee, ogopa Kanyaboya eee.” Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo.

Juwata Jazz Band nao walitunga wimbo mmoja waliouita ‘Kanyaboya’, ingawa huu ulikataliwa kurekodiwa Redio Tanzania Dar es Salaam. Sijui kwa nini? Labda baadhi ya maneno hayakuwapendeza, lakini ulikuwa ukipigwa kwenye kumbi mbalimbali ambazo bendi hiyo ilikuwa ikitumbuiza na kueneza elimu ya wananchi kuwa makini na ‘kanyaboya’

Wimbo uliitwa hivyo hivyo ‘Kanyaboya’ “Wacha kuuzia watu magunia, wacha kanyaboya utaumia.” Hayo ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye kibao hicho.



Jinsi walivyokuwa wanatapeliwa ni pale mtu anapokwenda kutaka kuuziwa shati, suruali au viatu.

Anakutana na mtu kasimama na shati, suruali au viatu, anauza kwa bei rahisi, tofauti na ile inayouzwa kwenye meza ya bidhaa.

Baada ya kupatana bei, wakati mteja anatoa pesa mfukoni, muuzaji naye anafunga mzigo kwenye kifurushi, na hasa ilikuwa kwenye gazeti kwanza, halafu unawekwa kwenye mfuko wa karatasi.

Lakini wakati huo huo, wakati anafunga, kuna mtu mwingine wa akiba ambaye mnunuzi huwa hamuoni. Yeye anakuwa na mfuko khaki unaofanana kabisa ule alioshika mwenzake.

Kutokana na kuwa na watu wengi maeneo ya soko, au mahitaji ya nguo, wanabadilishana mfuko bila mnunuzi kujua.

Anapita nyuma ya mwenzake na kubadilishana mifuko bila kuonekana kwa urahisi kutokana na mwingiliano mkubwa wa watu. Ule mfuko wenye shati, suruali au viatu ambavyo mteja ameviona na kukubali kununua, unachukuliwa na mtu mwingine na yule jamaa anampa mfuko ambao una magunia mabovu, matambara au kabishi lililochongwa mithili ya viatu.

Kwa sababu mteja anakuwa ameshaonyeshwa bidha anakuwa hana muda tena wa kuangalia, badala yake mawazo yake yanakuwa kwenda kutafuta usafiri wa nyumbani, ili kwenda kujaribisha nguo yake, akiwaza jinsi atakavyowakoga wenzake.

Taharuki inakuja anapofika nyumbani, atakapofungua na kukuta ameuziwa magunia, matambara mabovu, au kabichi lililochongwa. Hapo ndipo anapotambua kuwa amepigwa ‘kanyaboya’.

Wengi walikuwa wanadhani kuwa watu hao ni ‘wachawi’. Ukweli ni kwamba wana mbinu kali ambazo ukiwa mtu wa papara ni lazima ulie tu.

Hata ukienda kesho sehemu ile ile huwezi kumkuta. Utamkuta mtu mwingine kabisa.

Hiyo ndiyo ‘kanyaboya’. Utapeli ambao ulipamba moto miaka hiyo, na sababu kubwa ilitokana na uhaba wa nguo nchini Tanzania uliosababishwa na mdororo wa uchumi, hasa baada ya vita ya Kagera.

Lakini cha kushangaza hata miaka ya hivi karibuni tu kuna watu walikuwa wanauziwa miche ya sabuni, wakiambiwa ni simu za mkononi. Wizi huu ulienea pale Ubungo, kulikokuwa Kituo Kikuu cha Mabasi ya kwenda Mikoani, ambapo kwa sasa kimehamia maeneo ya Mbezi.

Nakaribisha maoni kwa mtu yoyote ambaye aliwashawahi kukutana na aina hii ya wizi, yeye mwenyewe, ndugu au mtu wake wa karibu na yatachapishwa wiki ijayo.

**Tuma meseji 0716350534**



# Israel yasema haitakalia eneo ukanda wa Gaza

**TEL AVIV,** ISRAEL

HATIMAYE Waziri mkuu wa Israel amesema nchi yake haitaki kuliteka, kukalia au kutawala eneo la Ukanda wa Gaza baada ya kumalizika vita na Hamas.

Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu alikiambia kituo cha televisheni cha Marekani Fox News kwamba nguvu ya kuaminika itahitajika kuingia katika eneo hilo ikiwa ni lazima ili kuzuia kuibuka kwa vitisho vya wanamgambo.

"Hatulengi kuteka Gaza, hatutaki kuikalia Gaza, na hatutaki kuitawala Gaza," alisema.

Aliongeza kwamba kuwa serikali ya kiraia itahitajika kutawala eneo hilo, lakini Israeli pia itahitaji hakikisho kwamba shambulio kama lile la Oktoba 7, ambalo Hamas walilifanya na kuua watu 1,400, halitokei tena.

"Kwa hiyo, tunapaswa kuwa na kikosi cha kuaminika ambacho, ikibidi kitaingia Gaza na kuwaua wauaji kwa sababu hilo ndilo litakalozuia kuibuka tena kwa kundi linalofanana na Hamas," alisema.

Maoni hayo ya Netanyahu yalikuwa yamependekeza kuwa Israeli itawajibika kiusalama huko Gaza. Aidha, Marekani imesema Israel itaanza kutekeleza usitishaji wa mapigano kwa saa nne kila siku katika maeneo ya kaskazini mwa Gaza.

Msemaji wa Baraza la Usalama la Kitaifa la Marekani John Kirby alisema hatua hiyo itachukuliwa ili kuwapa nafasi watu wanaotaka kuondoka kwenda kusini mwa Gaza kufanya hivyo.

Hata hivyo, Waziri wa Ulinzi wa Israel alisisitiza kuwa hatua hiyo ni za ndani na kubainisha kuwa hazitazuia mapigano.

Awali, Rais Biden alisema kutakuwa na njia mbili za kibinadamu zinazoruhusu watu kuondoka katika maeneo ya mapigano.

Siku ya Alhamisi mapigano makali yaliripotiwa karibu na hospitali mbili kubwa katika Jiji la Gaza. Rais Biden pia alisema Marekani inajaribu kuongeza vifaa vya kibinadamu na usaidizi kwa Gaza. Alisema analenga kuingiza lori 150 za msaada kila siku katika eneo hilo.

Hata hivyo, Umoja wa Mataifa ulisema kiasi cha misaada inayoingia Gaza ilikuwa inakidhi sehemu ya mahitaji ya watu na hali ya kibinadamu imekuwa ngumu na haivumiliki.

Israel imekuwa ikishambulia kwa mabomu Gaza kwa zaidi ya mwezi mmoja na ilianza mashambulizi makubwa ya ardhini wiki mbili zilizopita kwa lengo la kuwaangamiza wanamgambo wa Hamas.

Vita hivyo vilianza Oktoba 7, baada ya wanamgambo wa Hamas kuvuka mpaka na kufanya shambulio ambalo halijawahi kushuhudiwa kusini mwa Israel.

Wizara ya afya ya Gaza inayosimamiwa na Hamas ilisema watu 10,800 wameuawa katika eneo hilo tangu mashambulizi makali yalipoanza na wengine milioni 1.5 wakikimbia makazi yao.

Katia hatua nyingine, Kansela Olaf Scholz alissema anafedheheka na kughadhabishwa na mashambulizi ya chuki ya hivi majuzi dhidi ya Wayahudi nchini Ujerumani.

Wakati mapigano yakiendelea kati ya Israel na Hamas, mifarakano ya kijamii imaeanza kuibuka nchini Ujerumani.

Hofu kuhusu kuongezeka kwa chuki dhidi ya Wayahudi, tangu kuzuka kwa uhasama kati ya Hamas na Israel, unazidi kuenea nchini kote.

Ndani ya Ujerumani, matukio mbalimbali ya chuki kama vile ya kurushwa kwa mabomu mawili ya petroli kuelekea kwenye sinagogi la Berlin yameripotiwa na kuibua hofu ya kuenea kwa siasa za nazi.

**BBC**



Wapalestina wakikimbia mapigano kuelekea upande wa kusini mwa Gaza ambako kuna usalama.
**PICHA: AP**

## Mauaji Darfur yaongezeka

**KHARTOUM,** SUDAN

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la uhamiaji limesema watu takribani 700 waliuawa katika eneo la Darfur Magharibi mwa Sudan kufuatia mapigano kati ya jeshi na vikosi vya RSF.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki iliyopita huko El Geneina ambapo watu wengine 300 wanaripotiwa kutoweka.

Shirika la haki za binadamu la eneo hilo linakadiria kuwa watu 1,300 waliuawa Darfur Magharibi tangu Ijumaa iliyopita na ililaumu kikosi cha RSF kwa kuhusika na mauaji hayo.

Haya yanajiri huku wanamgambo wa RSF wakionekana kuongeza kasi ya mashambulizi katika kanda hiyo. Mashahidi walishutumu kundi hilo la wanamgambo na washirika wake kwa kuwalenga watu wasio Waarabu katika maeneo ambayo imeyateka.

Shirika la Roots Organization for Human Rights and Violions Monitoring, kundi linalotetea haki za binadamu huko Darfur Magharibi, linaituhumu RSF kwa kuvamia kambi za wakimbizi na kuanzisha mashambulizi.

Hata hivyo, RSF ilikanusha shutuma hizo.

Kulingana na mashirika ya misaada, maelfu ya watu wamekimbilia nchi jirani ya Chad katika siku za hivi karibuni.

Zaidi ya watu milioni tano na nusu wanakadiriwa kukimbia makazi yao tangu kuanza kwa ghasia kati ya RSF na Vikosi vya Wanajeshi wa Sudan mwezi Aprili mwaka huu.

**BBC**

## Rais Somalia afanyiwa upasuaji

**MOGADISHU,** SOMALIA

RAIS wa Somalia Hassan Sheikh Mohamud amefanyiwa upasuaji wa bega akiwa katika nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) hivi karibuni.

Taarifa ya ofisi ya rais iliyotolewa juzi ilisema Mohamud alipata nafuu baada ya upasuaji huo mdogo.

Hata hivyo, haikutoa maelezo zaidi juu ya kuumwa kwa kiongozi huyo.

Rais huyo alikaa Abu Dhabi kwa siku chache na alikutana na maofisa wakuu wa UAE, lilisema Shirika la Habari la Kitaifa la Somalia (Sonna).

Baada ya matibabu hayo, Rais Mohamud alisafiri hadi Riyadh, nchini Saudi Arabia, kuhudhuria mkutano wa kilele wa kati ya Saudi na Afrika.

Tangu kuchaguliwa tena mwaka jana, Rais Mohamud amesafiri katika mataifa kadhaa, yakiwemo mataifa ya Ghuba, kutafuta uungwaji mkono katika mapambano dhidi ya kundi la al-Shabab.

**DW**

## Chanjo Chikungunya yaanza rasmi

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeidhinisha kufanyika zoezi la uchanjaji wa mara ya kwanza duniani dhidi ya homa ya Chikungunya.

Kulingana na mamlaka inayosimamia chakula na dawa ndani ya nchi hiyo, (FDA) ya Marekani, imekubali kutumika kwa chanjo hiyo ambayo imepewa jina la Ixchiq iliyotengenezwa na kampuni ya Ulaya, inayoitwa Valneva.

Hata hivyo,imeidhinishwa kutolewa kwa watu wenye umri wa kuanzia miaka 18 na zaidi walioko katika hatari ya kuambukizwa.

Uidhinishwaji wa chanjo hiyo unatarajiwa kuharakisha usambazwaji wa dozi za chanjo hiyo katika nchi ambazo virusi hivyo vimeenea zaidi hasa Afrika, kusini mashariki mwa Asia na nchi za Amerika. Chikungunya, husababisha homa na maumivu makali ya viungo. Virusi vyake huenezwa na mbu na wataalam wa dawa wanataja kuwa tishio la afya linaloongezeka duniani.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**EMMANUEL D. MKINGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba : **S0179-0007** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST MARY'S SEMINARY MBALIZI** mwaka 2007 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0121-0508** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST JAMES SECONDARY SCHOOL** mwaka 2010. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/28641/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**EMMANUEL D. MKINGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo cha Degree chenye usajili namba **BAC/10/50119** kilichotolewa na CHUO CHA IFM mwaka 2013 na cheti cha **MASTERS DEGREE** chenye jina la **EMMANUEL DISMAS MKINGA** chenye usajili namba **IMC/MFI/16/90879** kilichotolewa na chuo cha IFM mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chocote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/28641/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NESTORY PAULINE MTONGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 779 DMF.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/37222/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IDDY KESSY KIRUME** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye jina la umiliki **ABDALLAH JUMA KADONO , USAJILI NAMBA, T 892 AUW,** CHASSIS NAMBA:**BHW41705036** na ENGINE NAMBA: **TD42163778.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/ILA/32911/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ETINESS THIOBIAS KIMARIO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA VEROSSA** yenye usajili namba **T 797 DFE,** CHASSIS NAMBA: **GX1106060096** na ENGINE NAMBA: **1G6967997.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/6758/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**
**ILIYOPO WILAYA YA MOROGORO**

**SHAURI LA MAOMBI MADOGO NA. 14/2023**

**NEEMA SIMON MAYBA..............................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**LUKANGA BIGAMBO..........................MJIBU MAOMBI**

### WITO/KUITWA SHAURINI KWA LUKANGA BIGAMBO

POPOTE ULIPO unatakiwa ufike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro tarehe 27/11/2023 saa 2:30 asubuhi ambapo shauri lako limepangwa kutajwa
Endapo hutofika wewe binafsi ama mwakilishi wako shauri tajwa litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Imesainiwa leo tarehe 03 Mwezi 11 Mwaka 2023

E. USHACKY
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA ARDHI NA. 10/2022**

**SAIDI MBONDE...................MLALAMIKAJI**

**DHIDI YA**

1. **LINDI MUNICIPAL COUNCIL..................MLALAMIKIWA**
2. **DOMINICK JOHN NGOLEKA..................MLALAMIKIWA**
3. **YUSUFU LIKOKO..................................MLALAMIKIWA**
4. **HAMISI ABDALLAH..............................MLALAMIKIWA**
5. **ALLY SELEMANI SIMBA.......................MLALAMIKIWA**
6. **THE ATTORNEY GENERAL...................MLALAMIKIWA**

### KUITWA SHAURINI

**KWA: YUSUFU LIKOKO – POPOTE ULIPO TANZANIA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama Kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe 6/12/2023 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.
Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi rufaa hii itasikilizwa na kuariwa bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 01/11/2023.

F.R. LUKUNA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA ARDHI NA. 10/2022**

**SAIDI MBONDE...................MLALAMIKAJI**

**DHIDI YA**

1. **LINDI MUNICIPAL COUNCIL.................MLALAMIKIWA**
2. **DOMINICK JOHN NGOLEKA..................MLALAMIKIWA**
3. **YUSUFU LIKOKO..................................MLALAMIKIWA**
4. **HAMISI ABDALLAH..............................MLALAMIKIWA**
5. **ALLY SELEMANI SIMBA.......................MLALAMIKIWA**
6. **THE ATTORNEY GENERAL...................MLALAMIKIWA**

### KUITWA SHAURINI

**KWA: ALLY SELEMANI SIMBA – POPOTE ULIPO TANZANIA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama Kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe 6/12/2023 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.
Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi rufaa hii itasikilizwa na kuariwa bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 01/11/2023.

F.R. LUKUNA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA ARDHI NA. 10/2022**

**SAIDI MBONDE...................MLALAMIKAJI**

**DHIDI YA**

1. **LINDI MUNICIPAL COUNCIL...........MLALAMIKIWA**
2. **DOMINICK JOHN NGOLEKA...........MLALAMIKIWA**
3. **YUSUFU LIKOKO...........................MLALAMIKIWA**
4. **HAMISI ABDALLAH.......................MLALAMIKIWA**
5. **ALLY SELEMANI SIMBA................MLALAMIKIWA**
6. **THE ATTORNEY GENERAL............MLALAMIKIWA**

### KUITWA SHAURINI

**KWA: HAMISI ABDALLAH – POPOTE ULIPO TANZANIA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama Kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe 6/12/2023 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.
Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi rufaa hii itasikilizwa na kuariwa bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 01/11/2023.

F.R. LUKUNA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie*

***0745 700 710.***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha umama wa nyumba asiyojenga, ndiyo akawa sasa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa wakiishi bure na mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo hadi mwisho wa visa vya mama huyu.

## MAMA MWENYE NYUMBA-1

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"He! Yaani humu ndani mpaka saa hizi hakujafagiliwa! Nje kuchafu, chooni kuchafu, imekuwaje?"

Alikuwa na mama mwenye nyumba, Mwantumu ambaye alikuwa ametoka chumbani kwake, akazunguka eneo lote la nyumba yake. Akaenda chooni. Alipotoka ndipo alipoanza kubwata.

Baada ya kuona hajajibiwa aliongeza sauti.

Jamani ee humu ndani nani mwenye zamu ya kufagiaaa."

Kabla hajajibiwa, dada mmoja wa chumba kingine alifungua mlango. Alikuwa amevaa khanga tu. Alionekana ametoka kulala na kelele za mama mwenye nyumba ndizo zilizomshtua,

"Mama eee koromelo lisikutoke kama ndege korofindo, mwenye zamu ya kufagia Devota!"

Mwantumu alimtazama kwa jicho kali lakini hakumjibu kitu. Lilionekana kabisa likimwambia, "wewe bado zamu yako."

kwenye chumba cha mpangaji wake huyo. "We Devota amke uje utufagilie huku wenzio, tunaamka uwanja mchafu, chooni nako kuchafu, aaa, kwanza mwanamke gani unalala mpaka saa hizi?"

Ghafla mlango ukafunguliwa. Akatoka mwanamke mmoja asiyezidi miaka 26, mrefu mwembamba, na mweupe wa kununua dukani. Nywele zake nyingi zilikuwa timtim na hiyo ni kwa sababu ndiyo kwanza anaamka. Hajaziseti, au kuweka dawa, mafuta na vikorombwezo vingine.

"Jamani watu tumelala mnatupigia makelele kwa nini lakini? Nyumba kama tunakaa bure!"

"Lo! Amka ufanye usafi, unalala tu kama pono tu! Wewe kila siku ikiwa zamu yako matatizo, mbona wenzako ikifika zamu hao hakuna kelele, ila wewe tu!"


"Mmmh! Nyumba ina kelele hii!"

"Kapange Oysterbay kama unaona hapa kuna kelele, wezako si wamepanga huko 'apatmenti', we unasubiri nini? Mchafu mkubwa we."

"Wewe unayeniambia mimi mchafu, wewe una usafi gani, hata kuoga hujui. Kutwa nzima miguu imekupauka kama mbeba mifuko ya simenti."

"Wewe ndiyo unajua kuoga, minywele tu kama zombi, acha uchafu, mwanamke unalala mpaka saa tano tusikwambie kwa nini?"

"Sasa nasema hivi, kufagia sifagii na hamnifanyi kitu." Mpangaji akaonekana kukasirika.




**"Wewe mwenyewe unajua bei yake? Mama yako ndiye aliyekuwa anajua bei yake siyo wewe."**

"Weweee, weweee, nasema utafagia, kila siku wenzako tunafanyia zamu, wewe ikifika zamu yako unakwepa, kiangalie vile."

"Wewe huwa unafagia? Lini umefuata zamu ya kufagia ilivyo. Umeweka zamu, lakini wewe ndiyo unayeivuruga kwa sababu mama mwenye nyumba. Unafagia siku ukijisikia, siku ukila vizuri nyama, samaki wali, na ukiwa na hela hapo, lakini ukiwa huna hela unanuna na kufagia hufagii."

"We Devota usinizoee, mimi siyo mama yako au dada yako, na kodi yako ikiisha safari hii uondoke, sitaki tena ukae hapa."

"Siyo kodi yangu ikiisha, we nirudishie tu pesa yangu uone kama nitakaa hapa, nani anataka kuishi kwenye nyumba kama hii. Kwanza kijumba chenyewe kibovu, basi mkae kwa amani mdomo mdomo, mvua ikinyesha juu kunavuja..."

"Ndiyo nishasema hivyo, imebaki miezi sita, uondoke, tumekuchoka."

"Wewe mwenye tumekuchoka wapangaji wote, mama gani mdomo mdomo, umbea umbea..."

"Bibi wee, unatuchelewesha, kafanye usafi."

"Nitafanya kwa wakati wangu," akajibu mpangaji huyo na kufunga mlango kwa nguvu.

"Wee unanivunjia mlango wee, unajua bei yake?"

"Wewe mwenyewe unajua bei yake? Mama yako ndiye aliyekuwa anajua bei yake siyo wewe."

Haya ndiyo maisha ya nyumba namba 14, Magomeni Makuti, jijini Dar es Salaam kwenye nyumba ya Mwantumu.

Alikuwa akijibizana na mpangaji Devota aliyeonekana hajali hili wala lile.

Kuna maeneo ambayo Devota alikuwa akipiga ikulu, kwani ni kweli haikuwa nyumba ya Mwantumu bali ni ya marehemu mama yake aliyefariki miaka sita iliyopita na kuwaacha watoto wawili wasichana, Mwantumu na mdogo wake Tatu.

Tatu yeye ameolewa Sinza. Awali nyumba hiyo ilikuwa na wapangaji watupu, Mwantumu akiwa na kazi ya kuja kuchukua kodi tu, akiwaacha wapangaji wakiishi kwa raha na amani.

Wapangaji walikuwa wakisaidiana kwa shida na raha. Mmoja akipika maharage mwingine nyama, na mwingine mboga za majani, kila mmoja anajikuta ni kama amepika mboga nne au tano kwa sababu wanapeana.

Siku mmoja akiwa hana hela, basi mwenzake akipika chakula mchana anamwita yeye na watoto wake, au anakopeshwa pesa, au kupewa unga.

Tangu Mwantumu atue pale, kila kitu kimevurugika. Amewatawanya, amewagombanisha na kutoa vinenoneno mpaka kila mmoja amebaki kivyake.

Wanasalimiana na kuongea kwa sababu tu wote wanaishi nyumba moja, lakini ile kuishi kijamaa na kindugu kama zamani hakuna tena.

Miaka miwili tangu arudi pale imekuwa kama mwiba kwa wapangaji. Aliamua kurejea kwenye nyumba ya mama yake baada ya kuachika kwa mumewe.

Alikuwa akiishi Kigogo Sambusa na mumewe, lakini akachoshwa na mambo yake, kusutwa kila kukicha, mume akirudi mara amkute amepata kipigo kutoka kwa wanawake wenzake ambao hawawezi kuvumilia kusikia wanasingiziwa mambo ambayo hayapo.

Mume akaona ya nini? Akaamua kumpa talaka. Akarejea nyumbani. Wapangaji sasa wakaanza kuonja adha ya kuishi na mama mwenye nyumba.

Tabia ni kama ngozi ya goti, haibadiliki. Ameendelea kuwa na tabia ile ile. Hata akipata pesa za kodi anashindwa kukarabati nyumba ambayo kila siku zinavyozidi kwenda inaendelea kuwa mbovu.

Mdogo wake Tatu analalamika kuwa hapewi pesa za kodi, badala yake dada yake anakula mwenyewe.

Mwantumu hampi pesa mdogo wake kwa sababu tu eti mumewe ana uwezo.

Anapopata pesa zake, atakwenda kununua kila kitu kizuri anachokiona, nguo, chakula kizuri, lakini jioni atakusanya shoga zake kwenda baa kunywa.

Zikiisha anafanya kazi ya kuombaomba na kuwasumbua wapangaji wake wa kiume wamkopeshe pesa.

Mwantumu ana watoto wawili wasichana ambao kila mmoja alizaa na baba tofauti.

Wote baada ya kumaliza kidato cha nne wapo nyumbani, na wamerudi kuishi hapo na mama yao.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AZAM KUSAKA MAKALI YA MTIBWA KWA GOR MAHIA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kurejea nyumbani na pointi sita kibindoni, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, ameanza maandalizi kwa ajili ya kuikaribisha Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Novemba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Ikimaliza mechi hiyo, Azam itabakia hapo kwa ajili ya kuwavaa KMC FC katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa Desemba 8, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili, Dabo alisema anahitaji matokeo mazuri katika michezo hiyo miwili na katika kuimarisha kikosi chake, anatarajia kutafuta mechi ya kirafiki ya kimatifa ili kuwaongezea mbinu wachezaji wake.

Dabo alisema tayari uongozi umeanza mazungumzo na Gor Mahia na endapo mambo yatakwenda vyema, vigogo hao kutoka Kenya watakuja nchini kucheza mechi hiyo ya kimataifa ya kirafiki.

Kocha huyo alisema baada ya mapumziko mafupi aliyowapa wachezaji wake, sasa wanarejea kambini ili kujinoa kwa lengo la kuhitaji kuvuna pointi kwenye mechi hizo mbili zinazofuata.

Alisema hana mchezaji ambaye ni majeruhi hivyo programu yake ya mazoezi itakwenda vyema kama alivyopanga.

"Nadhani kila mtu anaijua Gor Mahia ni timu kubwa na kwetu ni fursa kujiweka sawa kuboresha fikra zetu, kiwango chetu ni muhimu kwa mechi zijazo. Baada ya hapa tunakutana na mechi kubwa dhidi ya Mtibwa Sugar.

Ni muhimu sana kwetu kujiandaa na mazoezi magumu kuelekea mechi hiyo baada ya kupata matokeo mazuri katika michezo miwili iliyopita ya ugenini, tunahitaji kuendelea katika njia yetu hususani kuweka fikra zetu mbele," alisema Dabo.

Aliongeza kikosi chake kitacheza kwa nidhamu katika kila mechi na wanaziheshimu timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Hakuna timu ndogo, hakuna mechi nyepesi, tunaendelea kujiimarisha kwa sababu tunahitaji kupata ushindi katika kila mchezo tutakaocheza ama nyumbani au ugenini, kikubwa ni kuongeza utulivu," Dabo aliongeza.

Azam yenye pointi sawa na Simba iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara nyuma ya mabingwa watetezi, Yanga wakati Simba iko katika nafasi ya tatu.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Tambaza wakifanya maigizo ili kutoa elimu ya kuhamasisha ulipaji kodi katika mashindano maalum yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), yanayoshirikisha shule 59 kutoka Dar es Salaam na Pwani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# KMKM, Jamhuri hakuna mbabe

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA watetezi, KMKM SC wamelazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya Jamhuri ya Pemba katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A, juzi jioni.

Matokeo hayo yanaifanya KMKM ifikishe pointi 17 na kukaa katika nafasi ya tatu huku Jamhuri yenye pointi 10 iko kwenye nafasi ya 10 katika msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema mara zote unapokutana na timu ambayo ipo katika nafasi ya chini katika msimamo wa ligi huwa inacheza kwa kujihami ili kuhakikisha inapata matokeo mazuri.

Msimu alisema tangu awali walijua mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu wapinzani wao hawajafanya vizuri katika michezo iliyopita na juzi walihitaji kurekebisha makosa yao.

**Aliongeza timu zote ziliionyesha kandanda safi na kufanya mashambulizi ya kuviziana katika dakika zote za mchezo huo licha ya wachezaji wake kupoteza nafasi nyingi za wazi za kufunga dakika za lala salama.**

"Mchezo ulikuwa mgumu sana katika dakika zote, kipindi cha pili tulirudi kwa ari kubwa kuhakikisha tunapata alama tatu lakini ilishindikana kwa sababu washambuliaji wetu hawakuwa makini,"Msimu alisema.

KMKM itashuka tena dimbani kuvaana na JKU katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu Zanzibar utakaochezwa Novemba 20, mwaka huu.

# Morocco mambo magumu Geita FC

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutofanya vyema katika mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara, viongozi wa Geita Gold FC wameitisha kikao kujadili mwenendo wa timu hiyo, huku uamuzi wa kikao hicho ukitarajiwa kutangazwa kuanzia leo.

Mkurugenzi wa Geita Gold, Zahara Michuzi, alisema jana wameendelea na vikao kwa ajili ya kufanya tathmini ili kuangalia mwenendo wa timu yao tangu kuanza kwa msimu huu na kuongeza kikubwa ni kuwajadili waajiriwa wote ambao wako chini ya Kocha Mkuu, Hemed Suleiman 'Morocco.'

Zahara alisema hawafurahishwi na matokeo ambayo Geita Gold inayapata mpaka sasa katika ligi hiyo na wanataka kutumia muda wa mapumziko uliopo kutatua changamoto inayowakabili.

"Tumekuwa na vikao ambavyo vinahusu mwenendo mzima wa timu yetu, lengo ni kutoka mkiani na kufika sehemu tunayoitaka, tutatokeje, ndiyo maana tuna vikao, tukimaliza tutatoa mipango yote tuliyoipanga.

Katika vikao hivi hahusiki kocha tu, waajiriwa wa klabu wanahusika, hawa wote na benchi la ufundi ndiyo watatuambia nini shida na mwisho tutajadiliana na kutoa uamuzi," alisema Zahara.

Mkurugenzi huyo alidokeza huenda kipindi cha dirisha dogo wakafanya usajili wa kuongeza baadhi ya wachezaji wapya ili kukipa nguvu kikosi kilichopo.

"Kingine ni nia ya kikao ni kujipanga upya na kuangalia hata namna gani tutajiimarisha katika kipindi cha dirisha dogo la usajili, tunaweza kuongeza nguvu ili kufikia malengo tunayoyataka, lakini uamuzi kamili tutautangaza baada ya kukamilika kikao," alisema bosi huyo.

Hata hivyo taarifa za ndani zinadai huenda Morocco akatimuliwa katika kikosi hicho kinachotumia Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu baada ya kuona ameshindwa kufikia malengo ya klabu.

"Mtu wa kwanza ambaye nafasi yake iko hatarini kupoteza ni Kocha Morocco, ameshindwa kuipeleka timu katika malengo yake, wanasema ni vyema wakachukua uamuzi sasa kabla mambo hayajaharibika zaidi, hatutaki kusubiri msimu ufikie mwisho, tunajirekebisha mapema," kilisema chanzo chetu.

Geita Gold inashika nafasi ya 15 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imeshinda mechi moja tu kati ya michezo tisa iliyocheza na kutoa sare tatu, ina pointi saba kibindoni wakati Mtibwa Sugar yenye pointi tano inaburuza mkiani.



## ZISIKUPITE

### MBAPPE AGOMBEA ENGLAND

CHELSEA, Liverpool, Manchester United na Newcastle United zote zinaweza kutoa ofa za mkataba mpya kwa fowadi wa Ufaransa, Kylian Mbappe (24), ambaye ataingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na Paris St-Germain ifikapo Januari mwakani baada ya Real Madrid kuweka wazi haitamnunua mchezaji huyo. ***(FourFourTwo)***

### SPURS YASAKA MLINZI

KLABU ya Tottenham Hotspur itamlenga beki wa kati wa upande wa kushoto Januari baada ya kujua ukubwa wa jeraha la Micky van de Ven, huku beki wa Bournemouth, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 25 akitajwa. (***Standard)***

### VARANE NJIA MOJA

MLINZI wa Manchester United, Raphael Varane amehusishwa na kuhamia Saudia, lakini kocha Erik ten Hag anataka kubaki na Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 30.(***Football Insider***)

### ZUBIMENDI ANUKIA ARSENAL

MASKAUTI wa Arsenal walimtazama kiungo wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 24, wakati wa mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Benfica uliochezwa Jumatano iliyopita.(***90min)***

### TAREMI KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United inatazamiwa kufanya mawasiliano na FC Porto kuhusu uhamisho wa Januari wa kumnunua mshambuliaji wa Iran, Mehdi Taremi, mwenye umri wa miaka 31 ambaye anaweza kupatikana kwa euro milioni 10. ***(TeamTalk)***

### WIRTZ ASUBIRIWA EPL

LIVERPOOL na Chelsea lazima zisubiri hadi dirisha la usajili la majira ya joto iwapo wanataka kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa miaka 20 kutoka Bayer Leverkusen .(***TeamTalk***)

### GUIRASSY ATAKA SPURS

MCHEZAJI anayelengwa na Tottenham Hotspur, Serhou Guirassy (27) yuko tayari kuhamia Ligi Kuu England. Nyota huyo raia wa Guinea anafuatiliwa na klabu kadhaa, anapatikana kwa pauni milioni 15 kama kipengele cha kutolewa katika mkataba wake Stuttgart kinavyosema. ***(Guardian***)

### ARSENAL ILIFAULU KWA RAYA

ARSENAL ilizipiku Tottenham, Bayern Munich, Chelsea na Manchester United kumsajili mlinda mlango wa Hispania, David Raya mwenye umri wa miaka 28 kwa mkopo kutoka Brentford, kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo. (***Metro***)

### ROBINSON KUTUA VILLA

KLABU za Aston Villa na Southampton zinamfuatilia kiungo wa Derby County mwenye umri wa miaka 18 kutoka Ireland Kaskazini, Darren Robinson. (***Football Insider***)


### UNITED NA BOSI MPYA

SIR Jim Ratcliffe anatarajia kukamilisha ununuzi wake wa hisa asilimia 25 kwa Manchester United ndani ya siku chache zijazo na analenga kuanza jukumu lake jipya hapo Jumatatu. (***Sun***)

### HAG HATIMULIWI UNITED

MANCHESTER United kwa sasa haina mpango wa kuachana na kocha wake, Erik ten Hag licha ya timu hiyo kuanza vibaya katika mashindano mbalimbali msimu huu. (***Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PARTEY AJIPANGA KUONDOKA ARSENAL

**●●● Kiungo huyo aonyesha kutamani kujiunga na Juventus baada ya...**

**LONDON,** England

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ghana, Thomas Partey, amewaambia viongozi wa Arsenal anataka kuondoka katika dirisha la usajili Januari, 2024 litakapofunguliwa.

**Kiungo huyo mkabaji mwenye umri wa miaka 30, huu ni msimu wake wa nne akiwa na kikosi cha Arsenal baada ya kujiunga kwa ada ya pauni milioni 45 akitokea Atletico Madrid.**

Amefunga mabao matano katika mechi 104 na alikuwa na msaada mkubwa msimu uliopita wakati Arsenal ilipoonyesha nguvu kubwa katika mbio za kusaka ubingwa wa Ligi Kuu England.

Lakini, kwa sasa taarifa zinafichua Partey anataka kwenda kuanza maisha mapya kwa kubadili timu ifikapo Januari mwakani.

Kiungo huyo aliyecheza mechi 47 kwenye kikosi cha Ghana nusuru ashawishike na fedha za Saudi Arabia wakati klabu ya Al-Ahli ilipohitaji huduma yake katika dirisha lililopita la uhamisho wa majira ya joto na amekuwa akiwindwa pia na miamba ya Italia, Juventus.

Miamba hiyo ya Serie A ipo kwenye msako wa kiungo mkabaji na imepanga kufanya hilo kwenye dirisha la majira ya baridi na tayari mipango ya kumsajili Partey imeshaanza.

Partey mwenyewe yupo tayari kuhamia Turin, baada ya kupoteza namba kwenye kikosi cha kwanza cha Arsenal kufuatia ujio wa kiungo Declan Rice, aliyenaswa kwa ada ya pauni milioni 105 katika dirisha kubwa lililopita.

Partey, ambaye mkataba wake pale Emirates utafika tamati mwaka, 2025 anapiga hesabu pia kurudi kukipiga nchini Hispania.

# BABA WA DIAZ AACHIWA HURU




**LA GUAJIRA,** Colombia

SERIKALI ya Colombia ilithibitisha baba yake mshambuliaji wa Liverpool, Luis Díaz ameachiwa baada ya siku 12 za kutekwa kwake Kaskazini mwa Colombia na wanachama wa kundi la waasi la National Liberation Army (ELN).

Kuachiwa kwake kulitangazwa na ujumbe wa serikali ambao kwa sasa uko katika mazungumzo ya amani na kundi la waasi.

Díaz aliingia dakika 81 katika mechi ya Liverpool ikipoteza 3-2 dhidi ya Toulouse kwenye Ligi ya Europa saa chache baada ya baba yake kuachiwa na watekaji nyara.

Kabla ya mechi hiyo, kocha wake, Jurgen Klopp, alisema mshambuliaji huyo "amefurahishwa sana" na habari ya kuachiwa kwa baba yake.

"Inaonekana Diaz ana furaha sana," alisema Klopp akiiambia TNT Sports.

Utekaji nyara wa Luis Manuel Díaz ulifanyika Oktoba 28, mwaka huu katika mji aliozaliwa wa Barrancas ulivutia hisia za kimataifa haraka na kutoa wito wa kuachiwa kwake.

Jumapili iliyopita Diaz aliomba kuachiwa kwa baba yake baada ya kuifungia Liverpool bao katika mechi ya Ligi Kuu England akionyesha fulana iliyoandikwa "Uhuru kwa baba."

Baba yake Díaz, akiwa amevalia shati la kijani na kofia aliwapungia watu alipowasili katika mji wake wa La Guajira, akisindikizwa na maofisa wa usalama.

"Namshukuru Mungu kwa nafasi hii ya pili ya kunirejesha nyumbani, na niwashukuru watu wote wa Barrancas, La Guajira na Colombia kwa msaada mkubwa waliotoa kwa familia yangu," alisema.

Hapo awali haikufahamika ni nani aliyetekeleza utekaji nyara huo. Lakini serikali ya Colombia ilitangaza wiki iliyopita kwamba ilikuwa na habari kwamba baba yake Díaz alitekwa nyara na waasi wa ELN.

# Simeone ajifunga Atletico hadi 2027

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Atlético Madrid, Diego Simeone amesaini mkataba wa miaka mitatu wa nyongeza ambao utampeleka kukaa katika klabu hiyo hadi mwaka, 2027, imefahamika.

Simeone, ambaye aliteuliwa kuwa kocha mkuu wa Atletico Desemba, mwaka 2011, ndiye mwalimu aliyefanikiwa zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Katika miaka yake 12 ndani ya Atlético Madrid, ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu Hispania maarufu LaLiga, moja la Copa del Rey, Ligi ya Europa mara mbili, UEFA Super mara mbili na Supercopa moja ya Hispania.

Pia kocha huyo ameiongoza klabu hiyo kwenye fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Vyanzo viliiambia ESPN wiki iliyopita wakala wa Simeone ambaye pia ni dada yake, Natalia Simeone, walikutana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Atletico, Miguel Ángel Gil Marín kwa mazungumzo juu ya mkataba mpya wa kocha huyo.

Simeone alipokea ofa nono kutoka klabu ya Saudi Arabia, Al Ahli msimu uliopita wa joto, lakini vyanzo viliiambia ESPN upendeleo wake ulikuwa kubaki na timu ambayo aliichezea zaidi ya mechi 100 katika vipindi viwili kama mchezaji.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 53 alifundisha River Plate ya nyumbani kwao Argentina na alikuwa na muda mfupi katika klabu ya Italia ya Catania kabla ya kuchukua mikoba ya Atlético Madrid.





# United yapanga kumtoa Varane

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imepanga kumsajili beki wa kati wa Nice, Jean-Clair Todibo, ili awe mbadala wa mchezaji mwenzake raia wa Ufaransa, Raphael Varane ambaye anadaiwa huenda akatimkia Saudi Arabia katika dirisha lijalo la majira ya joto.

Ili kupata huduma ya Todibo mwenye umri wa miaka 23, taarifa zinadai Nice inahitaji pauni milioni 50 kwa nyota huyo ambaye mkataba wake unatarajiwa kumalizika ifikapo mwaka, 2027.

Varane mwenye umri wa miaka 30 amekuwa kwenye rada za vigogo mbalimbali vya Saudia Arabia tangu dirisha lililopita la majira ya joto, lakini Manchester United ilikataa kumuuza.

Hata hivyo, mpango wa United wa kutaka kuendelea kumtumia kwa sasa unadaiwa kubadilika kwa sababu beki huyo amekuwa akikumbwa na majeraha ya mara kwa mara katika kipindi cha hivi karibuni hali inayosababisha asipate muda mwingi wa kucheza.

Todibo tangu kuanza kwa msimu huu amecheza mechi 10 za mashindano yote na kutoa asisti moja wakati Varane naye amecheza mechi 10 za michuano yote.

## HABARI MICHEZO

# NDUMBARO AJITOSA SAKATA LA KIFUNGO CHA MWAKINYO

Na Saada Akida

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, ameagiza sakata la kufungiwa kucheza ngumi bondia, Hassan Mwakinyo, limalizike haraka kwa maslahi ya maendeleo ya mchezo huo.

Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), ilitangza kumfungia Mwakinyo kupigana ndani na nje ya nchi kwa muda wa mwaka mmoja pamoja na kulipa faini ya Sh. milioni moja baada ya kudai amekiuka taratibu.

Ndumbaro alitoa agizo hilo kwa Msajili wa Vyama vya Michezo, Evordy Kyando, baada ya kumalizika kwa kikao cha pande tatu kilichofanyika Novemba 7, mwaka huu.

**Kikao hicho kilimhusisha Mwakinyo, maofisa wa TPBRC na Kampuni ya PAF ambayo ilianda pambano ambalo bondia huyo alitakiwa kushiriki.**

Akizungumza na Nipashe jana, Ndumbaro alimtaka msajili kusimama katika falsafa ya wizara ambayo inaamini Sanaa, Muziki na Michezo ni ajira na uchumi na si sehemu ya matatizo au kufungiana.

Waziri huyo alisema anahitaji kupata mrejesho wa vikao ambavyo vinaendelea kati ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT), TPBRC, PAF na upande wa Mwakinyo huku akiamini pande hizo zitafikia mwafaka.

"Falsafa ya wizara inasema Sanaa, Muziki na Michezo ikiwamo ngumi ni ajira na uchumi, tunataka kuona tangu Mwakinyo alivyanza kucheza watu wangapi wamepata ajira kupitia yeye, ameingia kiasi gani na watu wake.

Tunataka kuona takwimu za vyama vyote wametengeneza ajira kiasi gani na uchumi, nitakuheshimu katika mambo hayo mawili 'ajira na uchumi' na sio kufungia watu au vyama na kubishana na watu," alisema Ndumbaro na kuongeza;

"Waambie vyama vyote wafanye tathmini wametengeneza ajira na uchumi kiasi gani, najua michezo sasa hivi inafuatiliwa ulimwenguni ukianzia mpira wa miguu na hata ngumi.

Unaona watu hawalali usiku wanafuatilia ngumi kwenye televisheni. Hatuko tayari kukaa na vyama ambavyo vinaleta migogoro, hivyo vinatakiwa kufutwa usajili na kuwapa wengine ambao tutakuwa nao sambamba," waziri huyo aliongeza.

Aliwataka wadau hao kuweka mbele maslahi ya taifa wakati wanajadiliana na hatimaye kupata hitimisho.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akizungumza na Hassan Mwakinyo (mwenye miwani), pamoja na viongozi wa BMT, Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC) na wawakilishi wa Kampuni ya PAF ambayo iliingia katika mgogoro na bondia huyo. **PICHA: SAADA AKIDA.**

# *JKT Queens katika kibarua kizito CAF*

Na Saada Akida

TIMU ya JKT Queens inatarajia kukutana na Sporting Casablanca kutoka Morocco katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo De San Pedro, Ivory Coast.

Wawakilishi hao wa Afrika Mashariki na Kati, JKT Queens ya Tanzania wanahitaji ushindi tu ili kufuzu hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ya kimataifa.

Tayari Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini inayoongoza Kundi B imeshasonga mbele baada ya kufikisha pointi sita. Kuelekea mchezo wa leo, Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya dhidi ya Sporting Casablanca.

Chabruma alisema mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wao pia wanahitaji ushindi ili kucheza hatua ya nusu fainali.

"Ni mechi muhimu sana kwetu, tumefanyia kazi changamoto zilizojitokeza katika mechi iliyopita, tumejiandaa vizuri na vijana wako tayari kupambana ili kupata ushindi ambao utatupeleka nusu fainali," alisema kocha huyo.

Aliongeza anaamini wachezaji wake wataongeza umakini katika mchezo huo kwa sababu wanataka kufikia malengo ya kubeba ubingwa wa michuano hiyo inayochezwa kwa mara ya tatu mwaka huu.

JKT Queens ilianza mashindano hayo kwa kupokea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Mamelodi Sundowns Ladies huku ikivuna pointi tatu muhimu kwa kuwafunga wenyeji, Athletic Abdijan mabao 2-1.

## Yanga: Tutaiadhibu zaidi Simba

INATOKA UK 24

Mwamnyeto.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipongeza Timu ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), inayosaka tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Dunia (U-20) na JKT Queens inayochuana katika Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake.

JKT Queens leo inavaa na Sporting Casablanca wakati Tanzanite kesho itawakaribisha Nigeria katika michuano hiyo ambayo fainali zake zitachezwa Paris, Ufaransa mwakani.

## Cadena atarajia mazuri Msimbazi

INATOKA UK 24

Ilikuwa lazima kufanya mabadiliko kipindi cha pili kwa kutoa viungo na kuongeza washambuliaji kwa sababu Namungo walikuwa nyuma muda mrefu na wanaacha nafasi," alisema Cadena.

Aliongeza kuingia kwa, Moses Phiri na Shaaban Chilunda, ni uamuzi uliosaidia kupatikana kwa bao la kusawazisha na ana matarajio ya kutumia wiki mbili kukisuka vizuri zaidi kikosi chake kwa ajili ya mechi ijayo ya kimataifa.

"Nitaendelea kubadilisha vitu vidogo na kuisuka timu ili kuwa imara zaidi kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yetu ikiwamo wa mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Asec Mimosas," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo FC, Denis Kitambi, alisema mchezo huo ulikuwa mzuri na amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kuvuna alama moja ugenini.

Alisema malengo ya timu yake katika mechi hiyo yalifanikiwa ingawa wenyeji waliwazidi kwa kufanya mashambulizi ya haraka na kufanikiwa kupata bao la kusawazisha katika kipindi cha pili na hatimate kugawana pointi.

"Mechi haikuwa rahisi na mabadiliko ya mapema niliyoyafanya na kuwapa nafasi Simba kupata bao la kusawazisha kwa kumtoa Manyanya (Hashim) na kuingia Majimengi (Hamad), unajua kuna muda walimu tunafanya maamuzi kulingana na presha ya mechi," Kitambi alisema.

Michezo

Jumamosi Novemba 11, 2023

Nipashe



Partey kuondoka Arsenal UK. 21



Ofisa Habari wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Ali Kamwe (kushoto) akiwa na Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally wakiwa Bungeni jijini, Dodoma jana. **PICHA: MTANDAO**

## Cadena atarajia mazuri Msimbazi

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Daniel Cadena, amesema sare waliyopata dhidi ya Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi hajaifurahia ingawa amesifia kiwango kilichoonyeshwa na nyota wake.

Simba ilisaka bao la kusawazisha katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na kuifanya ibakie katika nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Cadena alisema ameanza kufanyia kazi mapungufu mbalimbali aliyoyabaini ikiwamo kuimarisha safu ya ulinzi inayoruhusu bao katika kila mechi na kuwajenga washambuliaji kutumia vizuri nafasi wanazotengeneza.

Kocha huyo alisema jambo chanya kwake ni kuona wachezaji wameshika haraka mafunzo aliyowapa kitu ambacho anaamini kitasaidia kufanya vizuri katika mechi za mbele.

"Sijafurahia matokeo ya sare lakini nimependa jinsi tulivyocheza, kwa muda mfupi wachezaji wameshika mafunzo tulioyowapa, hilo ni jambo chanya kwangu.

INAENDELEA UK 23

# Yanga: Tutaiadhibu zaidi Simba

## ●●● Hersi atamba hawajaridhika, serikali yazipongeza Tanzanite, JKT Queens...

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Simba, uongozi wa Yanga umesema itafanya usajili 'mkubwa' katika kipindi cha dirisha dogo la usajili kwa lengo la kuboresha kikosi chao na kupata ushindi mnono zaidi watakapowavaa watani zao katika mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Lakini pia Yanga inapanga kujii marisha ili kufanya vizuri zaidi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, am bapo wameingia hatua ya makundi ikiwa ni mara ya kwan za baada ya miaka 25.**

Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema wanachama, mashabiki na wadau wa soka watarajie maingizo mapya ya wachezaji katika kipindi cha dirisha dogo kwa sababu wanataka kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kusonga mbele katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hersi alisema kila hatua wanayokwenda katika ligi na mashindano mengine wanayoshiriki ni ngumu na ili kufanya vizuri ni lazima wakiongezee nguvu kikosi chao.

"Dirisha dogo ni lazima kutakuwa na maingizo mapya kwa sababu tunaelekea kwenye hatua ngumu ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tumeshakaa na mwalimu ili kutupa mapendekezo ni sehemu gani anadhani zinatakiwa kuongezewa nguvu. Kwahiyo wanachama, mashabiki wa Yanga na wadau wote wa soka watarajie usajili mwingine wa nguvu kipindi hicho.

Naamini usajili huo utatufanya kuendelea kufanya makubwa, timu itafanya vizuri sana zaidi ya hapa, itakuwa bora zaidi ya hivi ilivyo, hizi tano tulizoziona zinaweza kuzidi katika mechi ya marudiano ya mzunguko wa pili," alisema Hersi.

Aliongeza siri ya mafanikio ambayo Yanga inayapata kwa sasa inatokana na utulivu wa wanachama na mashabiki wa timu hiyo unaowafanya viongozi kutekeleza vyema majukumu yao.

"Utulivu uliopo Yanga ndiyo unaotufanya na sisi kutekeleza mambo yetu vizuri, kukiwa na vurugu vurugu nje zinatufanya pia kupoteza maono na mwelekeo, kwahiyo nawashukuru Wana-Yanga kwa kuendelea kuwa na utulivu huu," alisema rais huyo.

Kuhusu mbio za ubingwa, bosi huyo wa Yanga alisema ni mapema sana kwa sasa na 'mwanga' utaonekana kuanzia kati ya Februari na Juni, mwakani kwa sababu kipindi hiko kutakuwa na mechi mfululizo ambazo zitasababisha Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa ngumu zaidi ya ilivyo sasa.

"Kuanzia Desemba tutakuwa na mechi za Ligi ya Mabingwa, Ligi Kuu na ikifika Januari pia itaongezeka michuano ya Kombe la Mapinduzi, ingawa mwezi huo kutakuwa na mapumziko ya kwenda AFCON kwa timu yetu ya taifa, ila Februari hadi Juni (kiasi cha miezi minne) tutacheza mfululizo kiasi cha mechi 18 za ligi.

Kumbuka hapo kuna Kombe la FA na baadhi ya mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, utaona ligi itakavyokuwa ngumu sana, kwa hiyo ni sasa ni mapema mno kuzungumzia ubingwa," Hersi alisema.

Naye nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, amesema wachezaji wote wa Yanga wanajipanga kujituma na kucheza katika kiwango cha juu kwenye kila mechi kwa sababu wanahitaji kubakisha ubingwa wa Bara klabuni kwao.

"Tumejipanga kucheza katika kiwango cha juu, tunajua kila mechi tunayocheza tunatakiwa kupata ushindi, hakuna mechi rahisi, hakuna timu ndogo kwenye ligi ya nyumbani au mashindano ya kimataifa, timu zote zilifanya usajili mzuri na zinaendelea kujiimarisha," alisema

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >